
ISBN 9966-9787-2-0

# YALE BIBLIA INAYOFUNDISHA



by
TOM SMALL

# YALE BIBLIA INAYOFUNDISHA

na

**TOM SMALL**

© Copyright 1985. 1997. 2003
Kenya Baptist Media
All Rights Reserved

Second Edition 1985

Third Edition 1997

Fourth Edition 2003

ISBN 9966-9787-2-0

Published by
Kenya Baptist Media
Thika Road, Ruaraka
P.O. Box 30370
00100-Nairobi

"Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake, naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao" (Ufunuo 21:3).

**2. Mbinguni ni mahali pa furaha ya milele.**

"Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita" (Ufunuo 21:4).

**3. Mbinguni kutakuwa mahali ambapo dhambi haitaingia.**

"Na ndani yake hakitaingia kamwe cho chote kilicho kinyonge, wala yeye afanyaye machukizo na uongo, wale walioandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo" (Ufunuo 21:27).

"Au hamjui ya kwamba wadhalimu hawataurithi ufalme wa Mungu?" (1 Wakorintho 6:9).

"Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake" (Ufunuo I:5).

Mkristo anaingia mbinguni kwa sababu Yesu amemuosha dhambi zake. Yesu alipokuwa msalabani alitwaa dhambi zetu juu yake mwenyewe. Na anatuvika katika neema yake.

**4. Mbinguni ni mahali pa kuabudu.**

"Nami sikuona hekalu ndani yake; kwa maana Bwana Mungu Mwenyezi na Mwana-Kondoo, ndio hekalu lake. Na mji ule hauhitaji jua wala mwezi kuuangaza, kwa maana utukufu wa Mungu huutia nuru, na taa yake ni Mwana-Kondoo. Na mataifa watatembea katika nuru yake. Na wafalme wa nchi huleta utukufu wao ndani yake" (Ufunuo 21:22-24).

**2. Jehanum ni mahali ambapo huwezi kuepuka.**

Mungu alitukabidhi sote rehema yake katika Kristo Yesu. Lakini mtu anapoishi na kufa hali anakataa mapenzi ya Mungu, hakuna matumaini kwake. Hakuna nafasi ya pili ama wokovu katika Jehanum.

"Na zaidi ya hayo, kati yetu sisi na ninyi kumewekwa shimo kubwa, ili wale watakao kutoka huku kwenda kwenu wasiweze; wale watu wa kwenu wasivuke kuja kwetu" (Luka 16:26).

**3. Jehanum ni mahali pa wale ambao wamekataa rehema ya Mungu katika Yesu Kristo.**

Mungu hapendi mtu ye yote kwenda jehanum. Kwa sababu ya upendo wake kwetu sisi, Mungu alitayarisha njia ya wokovu kwa kumtuma Yesu kuja kufa kwa ajili yetu. Mtu awaye yote apendaye njia za uasi na kukataa kutubu na kumwamini Yesu, basi afahamu wazi ya kwamba mshahara wa dhambi zake unakuja.

"Bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba" (2 Petro 3:9).

". . . asiyeamini amekwisha hukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu. Na hii ndiyo hukumu; ya kuwa nuru imekuja ulimwenguni, na watu wakapenda giza kuliko nuru, kwa maana matendo yao yalikuwa maovu" (Yohana 3:18-19).

## MBINGUNI

Biblia hufundisha mambo mengi ya kustaajabisha kuhusu mbinguni kuwa itakuwa shida kufikiria hayo yote katika nafasi hii ndogo. Walakini, tunataka kufikiria juu ya mambo yanayofuata:

**1. Mbinguni ni mahali alipo Mungu na Yesu Kristo.**

"Yesu akamwambia, Amini, nakuambia, leo hivi utakuwa pamoja nami peponi" (Luka 23:43).

"Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo" (Yohana 14:2-3).



# YALIYOMO

| SURA | UKURASA |
|---|---|
| 1. BIBLIA | 5 |
| 2. MUNGU | 11 |
| 3. BWANA YESU KRISTO | 18 |
| 4. ROHO MTAKATIFU | 23 |
| 5. DHAMBI NA SHETANI | 29 |
| 6. WOKOVU | 34 |
| 7. KANISA | 39 |
| 8. MAAGANO YA KANISA | 45 |
| 9. UWAKILI | 51 |
| 10. SIKU YA KUABUDU | 55 |
| 11. KURUDI KWAKE BWANA | 57 |
| 12. UFUFUO | 60 |
| 13. HUKUMU | 63 |
| 14. MAISHA YA MILELE | 65 |

## SURA YA 14

# MAISHA YA MILELE

Katika masomo yaliyotangulia tumeona jinsi Biblia inavyoeleza kuwako ufufuo wa watu wenye haki na wasio na haki. Pia tumejifunza kwamba hukumu itakuwako kwa watu wote.

Baada ya hukumu, kutakuwako na mahali pa kuishi milele mbinguni ama jehanum. Kila mtu ataishi mbinguni au jehanum. Kwa hiyo, ebu tuone jinsi Neno la Mungu linavyotufundisha juu ya mahali hapo pawili.

## JEHANUM

**1. Jehanum ni mahali pa kweli.**

Kuna watu wengine wanaokana kwamba hakuna mahali po pote pa mateso panapoitwa Jehanum. Mtu anaweza kukana kuwepo kwa jua, lakini lingali lipo. Biblia hufundisha wazi kwamba Jehanum ni mahali, na Yesu alikufa ili tupate kuepukana na Jehanum. Soma kwa uangalifu Luka 16:19-31 kabla ya kuisoma mistari mifupi iliyopo katika somo hili.

"Yule tajiri naye akafa, akazikwa. Basi, kule kuzimu aliyainua macho yake, alipokuwa katika mateso," (Luka 16:22-23).

"Nao hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele" (Mathayo 25:46).

"Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili" (Ufunuo 21:8)

"Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto" (Ufunuo 20:15).

"Watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake" (2 Wathesalonike 1:9).

imekuja ulimwenguni, na watu wakapenda giza kuliko nuru; kwa maana matendo yao yalikuwa maovu" (Yohana 3:18-19).

"Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawatarithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti, wala wevi, wala watamanio, wa watevi, wala watukanaji, wala wanyang'anyi" (1 Wakorintho 6:9-10).

"Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto" (Ufunuo 20:15).

## WATAKAOOKOKA WAKATI WA HUKUMU

Mtu hataokoka kwa sababu ya haki yake, bali awe ametubu, amempokea Yesu kama Mwokozi, na kusimama mbele ya Mungu katika wema ambao Yesu alikufa kumpatia.

"Asiyeamini amekwisha kuhukumiwa" (Yohana 3:18).

"Amini, amini, nawaambia, Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani" (Yohana 5:24).

"Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye" (2 Wakorintho 5:21).



## SURA YA 1

# BIBLIA

Kuna maswali mengine ambayo huulizwa mara nyingi yanayohusu Biblia. Katika somo hili tutafikiri juu ya maswali haya kwa uangalifu na tuone ikiwa tunaweza kupata jibu kwa kila moja.

## BIBLIA NI NINI?

Biblia ina vitabu vidogo vingi ambavyo vimewekwa pamoja ili kufanya kitabu kimoja kikumbwa. Tunapoanza kutazama ndani ya Biblia yetu, tutaona ya kwamba imegawanywa katika sehemu nyingi. Kila sehemu ina jina tofauti kama Mwanzo, Kutoka, Mathayo, n.k. Zamani za kale kila moja kati ya sehemu hizi 66 ilikuwa kitabu kimoja. Sasa vitabu hivi vidogo 66 vimewekwa pamoja na kuwa kitabu kikubwa kiitwacho Biblia.

Biblia ina migawanyiko miwili mikubwa. Mgawo wa kwanza una vitabu vya kwanza 39 vya Biblia na unaitwa Agano la Kale. Viliandikwa kabla ya kuzaliwa kwa Yesu. Mgawo wa pili una vitabu vya mwisho 27 vya Biblia, na unaitwa Agano Jipya. Viliandikwa baada ya kazi ya Yesu ulimwenguni.

Biblia ni kitabu cha zamani. Mwanzo, kitabu cha kwanza cha Biblia, kiliandikwa karibu miaka 1400 kabla ya kuzaliwa kwa Yesu. Ufunuo wa Yohana, kitabu cha mwisho cha Biblia, kiliandikwa karibu miaka 100 baada ya kuzaliwa kwa Yesu. Tunaona hapo kwamba vitabu hivi 66 viliandikwa zaidi ya muda wa karibu miaka 1500. Kitabu cha mwisho cha Biblia kiliandikwa karibu miaka 2000 iliyopita. Kwa kweli Biblia ni kitabu cha kizamani, lakini tunaona kwamba ujumbe wake ungali halali kama tangu kilipoandikwa. Itabaki kuwa ya haki wakati wote ujao.

## NI NANI ALIYEIANDIKA BIBLIA?

Hili ni swali ambalo husumbua watu wengine kwa sababu wamesikia kuwa watu kama Musa, Isaya, Paulo na wengine waliviandika vitabu vyote vya Biblia. Nyakati zingine inasemekana kwamba Biblia ni Neno la Mungu na ni Mungu aliyeiandika. Watu wengine hustaajabu jinsi Biblia inavyoweza kuwa Neno la Mungu iwapo iliandikwa na watu.

Pengine maelezo yanayofuata yatatusaidia kufahamu jinsi Biblia ilivyoandikwa na watu na hasa kuwa Neno la Mungu. Ebu tuchukue mfano kwamba jumbe wako anahitaji kukuandikia barua. Alimwita mwandishi wake na kumwambia yale yanayotakiwa kuandikwa. Mwandishi kwa uaminifu aliyaandika mambo hayo yote. Unapopata barua, utasema kwa haraka, "Nimepata barua kutoka kwa jumbe wangu." Ndivyo ilivyo na Biblia. Mungu, katika Roho wake Mtakatifu, aliwafundisha watu mambo ambayo yaliwalazimu kuandika na kwa uaminifu wake waliyaandika mambo hayo. Kwa hivyo tunapohojiana juu ya Biblia, twasema kwamba ni Neno la Mungu ingawaje mkono wa mtu uliyaandika maneno hayo. Kama barua ilikuwa ya jumbe, pia Biblia ni ujumbe wa Mungu kwa kila mmoja wetu.

## TUTAJUAJE KUWA BIBLIA NI KWELI?

Kuna sababu nyingi ambazo tunaweza kuamini kwamba ni kweli. Ebu kwanza tujifunze sababu hizi tatu.

**1. Tunaamini Biblia kuwa haki kwa sababu ya umoja wake.**

Tunapozungumza juu ya umoja wa Biblia huwa tuna maana gani? Ebu tufikirie juu yake katika njia hii. Tunaweza kuchagua watu karibu 40 na kuwagawanyia karatasi 66. Wengine watapata karatasi moja na wengine watapata zaidi. Baadaye kila mmoja aambiwe kwamba aandike hadithi moja kwa karatasi zao. Kisha watenganishwe ili wasiweze kujadiliana. Hakuna atakayejua ambayo mwenzake ataandika. Kisha tukusanye karatasi hizo tofauti zisomwe, na kuunganishwa pamoja sawasawa na kufanya hadithi moja kamili. Hatuna budi kusema kwamba hii haingeweza kutendeka isipokuwa mpaka mtu amemwambia kila mmoja atakachoandika.





# HUKUMU

Neno la Mungu hutuambia wazi kwamba siku inakuja ambayo Mungu atawahukumu watu wote.

"Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu" (Waebrania 9:27).

"Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu" (Matendo 17:31).

"Katika siku ile Mungu atakapozihukumu siri za wanadamu, sawasawa na injili yangu, kwa Kristo Yesu" (Warumi 2:16).

## WATAKAOFIKA MBELE YA HUKUMU

"Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya"
(2 Wakorintho 5:10).

"Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi" (Ufunuo 20:12a).

## WATAKAO HUKUMIWA

Mtu huwa chini ya hukumu ya Mungu kwa sababu ya dhambi zake. Hubaki chini ya hukumu ya Mungu kwa sababu ya kumkataa Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wake. Mtu anapokataa upendo na rehema za Mungu katika Kristo, huwa hawezi akasaidiwa. Wanaoishi na kufa kama wanamkataa Yesu kuwa Mwokozi wao wataadhibiwa katika hukumu.

"Asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu. Na hii ndiyo hukumu; ya kuwa nuru

"Tena, wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele, wengine aibu na kudharauliwa milele" (Danieli 12:2).

"Msistaajabie maneno hayo; kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu" (Yohana 5:28-29).

"Nina tumaini kwa Mungu, ambalo hata hao nao wanalitazamia, ya kwamba kutakuwa na ufufuo wa wafu, wenye haki na wasio haki pia" (Matendo 24:15).

## MATOKEO YA UFUFUO UJAO MAISHANI MWETU

1. **Hakikisho lenye furaha kwamba tunapokufa tutakuwa pamoja na Bwana wetu Yesu Kristo milele.**

"Kwa maana twajua ya kuwa nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tunalo jengo litokalo kwa Mungu, nyumba isiyofanywa kwa mikono, iliyo ya milele mbinguni" (2 Wakorintho 5:1).

"Lakini tuna moyo mkuu; nasi tunaona ni afadhali kutokuwamo katika mwili na kukaa pamoja na Bwana" (2 Wakorintho 5:8).

2. **Kujua ufufuo utakaokuja kunapaswa kutufanya kumtumikia Yesu Kristo kwa uaminifu.**

"Basi, ndugu zangu wapendwa, mwimarike, msitikisike, mkazidi sana kutenda kazi ya Bwana sikuzote, kwa kuwa mwajua ya kwamba taabu yenu siyo bure katika Bwana" (1 Wakorintho 15:58).



Sasa fikiria juu ya Biblia. Vitabu 66 vya Biblia viliandikwa zaidi ya muda wa miaka 1500 na watu wapatao 40. Hata hivyo vitabu hivi 66 viliunganishwa pamoja, na sasa vinaeleza hadithi moja ya Mungu, upendo wake, na njia yake ya wokovu katika Yesu Kristo. Biblia ilikuwa imeandikwa kwa wakati huo wote na watu wengi tofauti. Tunajua ya kwamba ni Mungu aliyemwambia kila mtu jinsi ya kuandika. Kwa sababu Mungu ndiye aliyewafundisha mambo ambayo wangeandika, kila sehemu huungana na nyingine sawa na kufanya hadithi kamili juu ya Mungu. Ingawa Biblia ina vitabu vingi tofauti, ni *kitabu kimoja* na kina *Mtungaji mmoja* – Mungu Mwenyewe. Hii ndiyo maana ya kusema umoja wa Biblia. Hasa umoja wa Biblia hutufanya sisi kuamini kuwa ni kweli.

2. **Tunaamini kwamba Biblia ni ya kweli kwa sababu huisemea mioyo yetu.**

Mtu akituambia ya kwamba mvua inanyesha na tunaweza kuiona, hapo tunatambua kuwa anasema ukweli. Kama macho yetu yanavyoweza kudhihirisha haki inayohusu mvua, Mungu ameiumba mioyo yetu ili itambue ukweli juu ya Mungu ikiwa tunataka hasa kujua. Yesu alitufundisha kwamba mtu anayetaka kweli kumjua Mungu ni mtu ambaye yuko tayari kufanya mapenzi ya Mungu jinsi yalivyofunuliwa kwake. Mungu atatusaidia kumjua ikiwa kwa uaminifu tunataka kutenda mapenzi yake.

"Mtu akipenda kuyatenda mapenzi yake, atajua habari ya yale mafunzo, kwamba yatoka kwa Mungu, au kwamba mimi nanena kwa nafsi yangu tu" (Yohana 7:17).

3. **Tunaamini Biblia kuwa ya kweli kwa sababu imejithibitisha yenyewe kuwa kweli.**

Ebu tufikirie njia mbili ambazo ndani yake Biblia hudhihirisha kuwa ya kweli. Kwanza, imejionyesha yenyewe kuwa ya kweli kwa kujisahihisha maelezo ya wakati ujao. Ingekuwaje ikiwa mtu angetokea na kutuambia kwamba vitu fulani vitatendeka siku zijazo. Ikiwa vitu hivi vingetendeka jinsi alivyosema, hapo tungetambua ya kuwa aliusema ukweli. Tunapata unabii katika Biblia yote. Kama tunavyosema historia ya Biblia, vitu ambavyo vilitangulia kusemwa ndani ya Biblia

vimekwisha tokea jinsi Biblia ilivyobashiri. Historia imethihirisha kuwa Biblia husema ukweli.

Pili, Biblia hujionyesha kuwa ya kweli tunapoujaribu ukweli wake. Ebu tufikirie juu yake katika njia hii – fikiria ya kwamba una gari. Siku moja gari hilo likaharibikia njiani. Hukujua namna ya kulitengeneza. Kisha mtu akatokea na kukuambia jinsi utakavyofanya ili uweze kulitengeneza gari hilo. Ulipomaliza kufanya vile alivyokwamuru, gari lilienda vyema tena. Ungetambua kwamba mtu huyo alikuwa ameusema ukweli kwa sababu gari lililotengenezwa limejaribiwa kwa ukweli wake. Ni sawa na Biblia. Maisha yetu yameharibiwa na dhambi. Tunaposoma, kuamini, na kuyatii mafundisho ya Neno la Mungu, tunaona kwamba kuna usalama mioyoni mwetu. Tena twajua kwamba Biblia ni ya kweli kwa sababu imejithibitisha kuwa ya kweli katika maisha yetu.

## MUNGU ALIMPA NANI BIBLIA?

Mungu alitoa Biblia kwa ajili ya watu wote. Biblia si kitabu cha nchi moja au kabila fulani. Agano la Kale kwanza liliandikwa katika lugha ya Kiebrania, na Agano Jipya liliandikwa katika lugha ya Kiyunani. Baadaye lugha hizi zikatafsiriwa kwa lugha nyingine kama Kilatini, Kiingereza, Dachi, Kireno, Kiswahili na Kinyakusa.

Lilikuwa kusudi la Yesu kwamba Injili iwe kwa ajili ya watu wote. Wakati ule ule kabla ya kwenda mbinguni alidhihirisha haya yote kwa wanafunzi wake. Aliwaambia, "Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari" (Mathayo 28:19–20).

## KWA NINI MUNGU ALITUKABIDHI BIBLIA?

Kuna sababu mbili kubwa zilizomfanya Mungu kutupatia Biblia. Ebu tufikirie sababu hizo kwa ufupi.



Tumaini letu la kufufuka hutegemea ufufuo wa Yesu na ahadi yake kwetu.

"Bado kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena; bali ninyi mnaniona. Na kwa sababu Mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai" (Yohana 14:19).

"Usiogope, Mimi ni wa kwanza na wa mwisho, na aliye hai; nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu" (Ufunuo 1:17-18).

**2. Mfano wa ufufuo wa Yesu:**

Kuna mambo mengi ambayo hatujafahamu kuhusu mwili wa Yesu baada ya kufufuka. Walakini, tunahitaji kufikiria kwa uangalifu mambo tunayoambiwa katika Biblia kuhusu mwili wake uliofufuka. Ulikuwa mwili ule uliozikwa katika kaburi uliofufuliwa.

"Hayupo hapa, amefufuka" (Luka 24:6a).

Mwili ule uliofufuliwa ulikuwa mwili wa kweli.

"Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nishikenishikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo" (Luka 24:39).

Mwili ule uliofufuliwa ulikuwa tofauti na miili yetu hapa ulimwenguni.

"Yakafumbuliwa macho yao, wakamtambua; kisha akatoweka mbele yao" (Luka 24:31).

Mwili ule uliofufuliwa ulitwaliwa mbinguni.

"Akiisha kusema hayo, walipokuwa wakitazama, akainuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao" (Matendo 1:9).

## KUFUFUKA KWA WATU WOTE

Kutakuwako na ufufuo wa waasi na wenye haki. Watu wengine hufundisha kwamba hakuna uhai tena baada ya kufa. Mungu, katika Neno lake, anatufundisha jambo tofauti.

## SURA YA 12

# UFUFUO

Tunaweza kufahamu vyema ufufuo wa Kikristo tukijifunza juu ya ufufuo wa Yesu. "Lakini sasa Kristo amefufuka katika wafu, limbuko lao waliolala" (1 Wakorintho 15:20). Wakati shamba la mahindi linapoanza kuiva, hindi moja litaiva kwanza. Na ndilo limbuko (yaani tunda la kwanza). Yale yatakayoiva baadaye yatakuwa kama lile la kwanza. Lakini tofauti itakuwa katika wakati – wala si katika aina. Ndivyo ilivyo na Kristo, limbuko la kwanza la ufufuo. Ufufuo wa Wakristo utafuata nao watafanana naye.

**1. Ukweli wa ufufuo wa Yesu:**

**Hakuna** swali juu ya ukweli kwamba Yesu aliangikwa msalabani. Alisulibishwa hadharani na matukano makubwa ulishuhudia. Maadui wake walijua kwamba amekufa. Askari waliofundishwa kazi ya kuwa katika zamu walimlinda waone kama amefariki kabisa. Alidungwa na mkuki ubavuni mwake kuhakikisha kuwa amekufa. Damu na maji yalipotoka, vilidhihirisha kufâ kwake. Wafuasi wapenzi wa Yesu hawangeweza kumchukua na kumweka kaburini kama kungekuwako na thibitisho la uhai katika mwili wake. Kifo cha Yesu kilikuwa wazi kwa kila mtu na hakukuwa na mashaka kwamba Yesu alikuwa amekufa. Vivyo hivyo ufufuo wake ulikuwa wa kweli. Ebu tufikiri juu ya Maandiko yanayotufundisha kuhusu kufufuka kwake.

"Wale aliowadhihirishia nafsi yake, kwa dalili nyingi, baada ya kuteswa kwake, ya kwamba yu hai, akawatokea muda wa siku arobaini, na kuyanena mambo yaliyouhusu ufalme wa Mungu" (Matendo 1:3).

"Na ya kuwa alimtokea Kefa; tena na wale Thenasara; baadaye aliwatokea ndugu zaidi ya mia tano pamoja; katika hao wengi wanaishi hata sasa, ila baadhi yao wamelala; baadaye akamtokea Yakobo; tena na mitume wote; na mwisho wa watu wote; alinitokea mimi, kama ni mtu aliyezaliwa si kwa wakati wake" (1 Wakorintho 15:5-8).



**1. Mungu alitoa Biblia ili wapotevu waweze kuijua njia ya wokovu na kuokolewa.**

Wakati Paulo alipomwandikia Timotheo, alizungumza juu ya Maandiko Matakatifu, akasema, ". . . ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu" (2 Timotheo 3:15).

"Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo" (Warumi 10:17).

Tunapaswa kufahamu siku zote ya kwamba ni Yesu ambaye hutuokoa. Biblia hutufundisha juu ya Yesu na jinsi ya kuokoka kwa imani.

**2. Mungu aliitoa Biblia ili waliookoka wajue jinsi ya kuishi kama Wakristo.**

"Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadhibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema" (2 Timotheo 3:16-17).

"Kwa mausia yako najipatia ufahamu, Ndiyo maana naichukia kila njia ya uongo" (Zaburi 119:104).

Kwa kuyafikiria maandiko haya twatambua jinsi Biblia inavyoridhisha kabisa kila hitaji letu la uongozi wa kiroho. Inatuonyesha njia ya wokovu na kutufundisha namna ya kuishi kama Wakristo.

## JE, TUSIKILIZE MAFUNDISHO AMBAYO YANAKANUSHA BIBLIA AMA YALE YANAYOONGEZEA?

Kuna sababu tatu muhimu sana za kutosikiliza mafundisho kama haya. Tukizijua sababu hizi, tutaona kwamba Mungu hutaka tuongozwe na Neno lake peke yake.

1. **Tusisikilize mafunzo kama hayo kwa sababu Mungu amejidhihirisha kabisa katika Yesu Kristo. Kwa hivyo haiwezekani kuwako na mafundisho makubwa kuliko haya kuhusu Mungu.**

Yesu alisema: "Aliyeniona mimi amemwona Baba; basi wewe wasemaje, Utuonyeshe Baba? Husadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu? Hayo maneno niwaambiayo mimi siyasemi kwa shauri langu; lakini Baba akaaye ndani yangu huzifanya kazi zake" (Yohana 14:9–10).

2. **Tusisikilize mafundisho ya namna hiyo kwa sababu Neno la Mungu ni kweli sasa kama tangu lilipoandikwa. Litakuwa kweli katika nyakati zijazo kama lilivyo siku hizi. Tena linatosha.**

"Majani yakauka, au lanyauka; Bali neno la Mungu wetu litasimama milele" (Isaya 40:8).

"Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayatapita kamwe" (Mathayo 24:35).

3. **Tusisikilize mafundisho ya namna hiyo kwa sababu Mungu atwambia katika kitabu cha mwisho cha Biblia kwamba hakuna kitakachoongezwa wala kuondolewa katika Neno Lake.**

"Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Na mtu ye yote akiondoa lo lote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki" (Ufunuo 22:18-19).

Tumshukuru Mungu kwa unyenyekevu kwamba ametuletea Neno Lake, ambalo ni Biblia. Ndani yake twaweza kufahamu njia ya wokovu na jinsi ya kuishi kwa kumpendeza Mungu. Basi tuisome, tuiamini, na tuitii.



# KUJITAYARISHA KWA KURUDI KWAKE

1. **Kujitayarisha kwa wale ambao hawajaokoka.**

Kuna kitu kimoja ambacho asiyeokoka anastahili kutenda ili ajiweke tayari kabla ya kuja kwake Bwana. Ni lazima atubu dhambi zake zote na kumkubali Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi. (Soma sura inayohusu wokovu.)

2. **Kujitayarisha kwa waliookoka.**

Mtu aliyeokoka lazima aishi kulingana na mapenzi ya Mungu kila siku ili kwamba, Yesu ajapo, amkute akiwa tayari.

"Kesheni basi; kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu" (Mathayo 24:42).

"Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi; katika siku hiyo mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu, na viumbe vya asili vitaunguzwa, na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea. Basi, kwa kuwa vitu hivi vyote vitafumuliwa hivyo, imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa, mkitazamia hata ije siku ile ya Mungu" (2 Petro 3:10-12).

"Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo. Na kila mwenye matumaini baya katika yeye hujitakasa, kama yeye alivyo mtakatifu" (1 Yohana 3:2-3).

## MATOKEO YA KUJA KWAKE

**1. Kuja kwake Yesu kutakuwa kwa maana gani kwa wale ambao hawajaokoka?**

"Wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake; katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake"
(2 Wathesalonike 1:7-9).

"Lakini mbingu za sasa na nchi zimewekwa akiba kwa moto, kwa neno lilo hilo, zikilindwa hata siku ya hukumu, na ya kuangamia kwao wanadamu wasiomcha Mungu" (2 Petro 3:7).

"Msistaajabie maneno hayo; kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu" (Yohana 5:28-29).

**2. Kuja Kwake Yesu kutakuwa na maana gani kwa waliookoka?**

"Msistaajabie maneno hayo; kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka, wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima" (Yohana 5:28-29).

"Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo" (Yohana 14:3).

"Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele" (1 Wathesalonike 4:16-17).



SURA YA 2

# MUNGU

Tunapojifunza juu ya Mungu, kwanza tufikiri habari ya kuwako Mungu. Si lazima tusome Biblia ili tujue Mungu yuko. Kuna watu wengine ulimwenguni ambao bado hawajaona Biblia, lakini wanafahamu kuna Mungu mkuu ambaye aliiumba mbingu na nchi. Ebu tujifunze sababu zinazofanya mioyo yetu kujua kwamba Mungu yuko.

**1. Uumbaji hutufundisha kwamba kuna Muumba.**

Tunapoangalia jengo kubwa, tunatambua kwamba halikutokea kwa ghafula. Fikiria juu ya vitu vyote vinavyopatikana ndani ya jengo hilo; msingi, maelfu ya matofali yaliyopangwa vyema, madirisha ya chuma, paa, vyumba na milango ya kupitia, na rangi iliyopakwa. Tunafahamu kwamba jengo kama hili lina mjenzi.

Katika hali hiyo jengo hili huhidhirisha kwamba lina mjenzi, na viumbe vyote hudhihirisha kwamba kuna Muumba. Tunao muumbo pamoja na miujiza yake, tunafahamu mioyoni mwetu kwamba mbingu na nchi hazikutokea kwa ghafla. Mtu fulani alivitengeneza. a mtu huyo ni Mungu.

"Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu, Na anga laitangaza kazi ya mikono yake" (Zaburi 19:1).

"Kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake; yaani, uweza wake wa milele na Uungu wake; hata wasiwe na udhuru" (Warumi 1:20).

**2. Njaa ya mtu kwa Mungu hutufahamisha kwamba Mungu yuko.**

Tunaishi katika ulimwengu ambao kuna jibu la njaa za mtu. Tumbo la mtu hutamani chakula, na huwako chakula cha kuishibisha njaa hiyo. Koo la mtu husikia kiu kwa kutaka maji, na kuna maji kwa ajili ya kutuliza kiu hicho. Macho ya mtu hushurutishwa kuwa na nuru ili yaweze kuona, na kuna nuru. Mwiti wa mtu huwa na shauku kwa vitu fulani na hapo tunapata majibu kwa shauku hizo zote.

Hata hivyo, moyo wa mtu husikia njaa ya kumtamani Mungu. aa hiyo hutufanya kutambua kwamba Mungu yupo ambaye huridhisha njaa ya mioyo yetu ya kumtafuta na kumjua.

"Kama ayala aioneavyo shauku mito ya maji. Vivyo hivyo nafsi yangu inakuonea shauku. Ee Mungu" (Zaburi 42:1).

**3. Kutambua dhambi kwa mwanadamu humwonyesha kwamba lazima aweko Mungu wa kutendwa dhambi.**

Ebu tufikiri kuwa kuna nchi ambayo haina mtawala au sheria ya kuitawala. Ungeweza kwenda katika nchi hiyo na kutenda unavyopenda, bila mtu ye yote kukwambia kuwa umevunja sheria ama wewe ni adui wà mfalme. Hapangekuwa na mfalme wa kutendwa dhambi. Lazima kuweko na mtu kabla ungeweza kumkosea yule mtu, tena ni lazima kuweko na sheria kabla ya kuzivunja hizo sheria.

Wakati mtu anapojiangalia kwa makini moyoni mwake, hujiona kwamba ametenda dhambi. Hujiona kuwa amefanya mambo ambayo ni mabaya. Hugundua kwamba amekosa kufanya mema yaliyompasa kutenda. Sasa, kwa kuwa ametenda dhambi, lazima aweko Mungu wa kutendwa dhambi. Lazima kuweko na amri za Mungu kabla ya kuzivunja. Ujuzi wa amri za Mungu umekwisha kuwekwa moyoni mwa binadamu na Mungu mwenyewe. Kwa sababu mwanadamu hufahamu ya kuwa ni mwenye dhambi twajua kuwako kwa Mungu tunayeweza kumtenda dhambi. Hakika haitulazimu kuwa na Biblia ili tujue kuna Mungu. Mungu mwenyewe ameiandika hekima hii mioyoni mwa watu wote.

"Hao waionyesha kazi ya torati iliyoandikwa mioyoni mwao" (Warumi 2:15).

## UTATU MTAKATIFU

Ingawa si lazima kuwa na Biblia ya kutujulisha kwamba kuna Mungu, Mungu alijua kuwa tunahitaji Neno kama hili ikiwa tungalifahamu vizuri tabia ya Mungu, njia ya wokovu, na njia ya maisha ya Kikristo. Sasa tutaanza kujifunza vile Biblia inavyotufundisha juu ya Mungu.



SURA YA 11

# KURUDI KWA BWANA

Mojawapo ya matumaini ya Wakristo ni kurudi kwa Bwana Yesu Kristo. Biblia pengine haitatwambia yote tunayopaswa kujua juu ya kurudi kwake, lakini yako mambo mengine yanayohusu kurudi kwake ambayo hatuna budi kuyajua.

## HAKIKISHO LA KURUDI KWAKE

"Kwa maana kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi, hivyo ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu" (Mathayo 24:27).

"Wakasema, Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni" (Matendo 1:11).

"Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu" (1 Wathesalonike 4:16a).

## KUTOKUUJUA WAKATI

"Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake" (Mathayo 24:36).

"Kesheni basi; kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu" (Mathayo 24:42).

"Lakini, ndugu, kwa habari ya nyakati na majira, hamna haja niwaandikie. Maana ninyi wenyewe mnajua yakini ya kuwa siku ya Bwana yaja kama vile mwivi ajavyo usiku" (1 Wathesalonike 5:1-2).

"Basi Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa Sabato pia" (Marko 2:28).

2. **Baada ya kupaa kwake mbinguni, Yesu alikuwako katika Roho Mtakatifu akiwafundisha na kuwaongoza wanafunzi.**

"Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake" (Yohana 16:13).

3. **Wanafunzi, chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, waliabudu katika siku ya kwanza ya juma. Hatuambiwi kwa nini walifanya hivyo, lakini tunajulishwa kuwa ndivyo walivyofanya.**

"Hata siku ya kwanza ya juma, tulipokuwa tumekutana ili kumega mkate, Paulo akawahutubu" (Matendo 20:7).

"Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake; ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja" (1 Wakorintho 16:2).

Tunaona kwamba makanisa ya Agano Jipya yaliabudu na kutoa vipawa vyao katika siku ya kwanza ya wiki. Tunapoabudu siku ya kwanza ya wiki, huwa tunaabudu siku ile, kama makanisa ya Agano Jipya yalivyokuwa yakiabudu. Mtu ye yote akisema hatutendi vema, anasema pia kwamba wanafunzi wa Agano Jipya walitenda vibaya. Tusiyasikize mambo kama haya, bali tuendelee kufuata mfano tunaopata katika Neno Takatifu la Mungu, Biblia.

## UTIMIZAJI SAWA WA SIKU YA KWANZA

Ingawa siku ya kuabudu ilibadilishwa, haja ya mwanadamu ingali kama vile ilivyokuwa. Angali anahitaji siku ya kupumzika na kuabudu. Siku ya kwanza ya juma imekuwa siku hiyo kwa Wakristo.

Mkristo anapaswa kufanya nini siku hiyo? Ni wakati wa kuhubiri Injili, wa kuabudu, na wa kupumzika. Mungu hapendi siku hii iwe siku nyingine ya kufanya kazi. Walakini, inafahamika kwamba riziki lazima ziangaliwe – kutibu wagonjwa, kulisha mifugo n.k. Ni lazima ujitahidi kutimiza yale ambayo Mungu amewekea siku hii. Ni siku ya kupumzisha mwili na kukuza roho.



Biblia hutufundisha juu ya Utatu Mtakatifu. Mafundisho yanayohusu Utatu Mtakatifu (Mungu hufunuliwa kama Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu) ni vigumu kuyaelewa. Hata hivyo, imedhihirishwa wazi katika Biblia. Haitupasi kufikiri kwamba kitu fulani si sawa kwa sababu tunakosa kukielewa kabisa. Kama mwandishi wa Zaburi alivyofikiria hekima ya Mungu, akasema, "Maarifa hayo ni ya ajabu, yanishinda mimi, Hayadirikiki, siwezi kuyafikia" (Zaburi 139:6.) Labda elimu ya Utatu haitashikwa kabisa, lakini inaweza kukubaliwa na kuaminiwa kwa sababu inafundishwa wazi katika Biblia.

Katika Biblia tunafundishwa kwamba kuna Mungu mmoja na mmoja tu. "Sikiza, Ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja" (Kumbukumbu la Torati 6:4). Biblia inadhihirisha wazi Mungu mmoja kama Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Basi tufikiri juu ya maandiko mengine yanayotwambia hivyo.

1. **Biblia hufundisha kwamba Yesu na Baba ni Umoja.**

"Mimi na Baba tu umoja" (Yohana 10:30).

"Aliyeniona mimi amemwona Baba; basi wewe wasemaje, Utuonyeshe Baba?" (Yohana 14:9b).

"Yaani, Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake" (2 Wakorintho 5:19a).

2. **Biblia hufundisha kwamba Yesu na Roho Mtakatifu ni Umoja.**

Kama Yesu alivyosema juu ya Msaidizi atakayekuja, Roho Mtakatifu, alithibitisha kuwako kwa Roho Mtakatifu na kuwako kwake kuwa sawasawa.

"Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele; ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu. Sitawaacha ninyi yatima; naja kwenu" (Yohana 14:16-18).

"Yesu akajibu, akamwambia, Mtu akinipenda, atalishika neno langu; na Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake" (Yohana 14:23).

**3. Biblia hutufundisha kuwa Mungu na Roho Mtakatifu ni Umoja.**

Petro alifundisha kwamba kumwambia Roho Mtakatifu uongo ni kumwambia Mungu pia.

"Petro akasema, Anania, kwa nini Shetani amekujaza moyo wako kumwambia uongo Roho Mtakatifu, na kuzuia kwa siri sehemu ya thamani ya kiwanja? Kilipokuwa kwako, hakikuwa mali yako? Na kilipokuwa kimekwisha kuuzwa, thamani yake haikuwa katika uwezo wako? Ilikuwaje hata ukaweka neno hili moyoni mwako? Hukumwambia uongo mwanadamu, bali Mungu" (Matendo 5:3-4).

"Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?" (1 Wakorintho 3:16).

Tukifikiria juu ya Maandiko yaliyo hapa juu, tunaona kwamba Biblia hutufundisha ya kuwa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni Umoja. Labda mfano utatusaidia kufahamu jinsi Mungu mmoja anavyoweza kuwa utatu ingawa hao ni mmoja. Ebu utazame mti. Ni mti mmoja, na kumbe mti huo una mizizi, shina, na majani. Kila sehemu ina kazi yake lakini ingali sehemu moja ya mti huo. Mungu ni Mungu mmoja, na amejifunua mwenyewe kuwa Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu.

## ASILI YA MUNGU

Kuna mambo mengi sana katika ulimwengu huu ambayo yamezidi akili ya mwanadamu. Ikiwa hatuwezi kuelewa mambo hayo ya ulimwengu, basi akili zetu haziwezi kumfahamu Mungu aliyeumba ulimwengu huu na vitu vyote. Hata hivyo kuna vitu tunavyoweza kufahamu juu ya Mungu kwa sababu amevifunua vitu hivyo katika Biblia. Basi na tufikirie juu ya mambo mengine ambayo Biblia hutufundisha kuhusu asili ya Mungu.

**1. Mungu ni wa Milele.**

Maana yake ni kwamba Mungu hana mwanzo wala mwisho. Amekuwapo siku zote na atakuwapo siku zote.



SURA YA 10

# SIKU YA IBADA

Yesu alithibitisha wazi kwamba sabato ipo ili kutimiza mahitaji ya mwanadamu.

"Akawaambia, Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya sabato" (Marko 2:27). Sasa tunaposoma Maandiko, tunapata kwamba sabato ilikusudiwa kutimiza mahitaji aina mbili katika maisha ya mwanadamu. Je, ni yapi?

**1. Mwanadamu anahitaji wakati wa kupumzisha mwili wake. Mungu alifanya siku ya sabato kuwa ya kupumzika.**

"Ikumbuke siku ya sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni sabato ya Bwana, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote" (Kutoka 20:8-10).

**2. Mwanadamu anahitaji wakati wa kuabudu na kupata mafunzo ya kiroho. Yesu alitumia sabato kwa kusudi hili na tena kama wakati wa kupumzika. Hii ilikuwa desturi yake.**

"Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa; na siku ya sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake, akasimama ili asome" (Luka 4:16).

Tunaona ya kwamba Mungu alipanga sabato kuwa siku ya kupumzika na kumwabudu.

## MAGEUZO YA SABATO KUWA SIKU YA KWANZA

Sisi kama Wabatisti, tunapaswa kufahamu vizuri sababu ya kuabudu siku ya kwanza ya juma badala ya siku ya saba. Jifunze kwa uangalifu mambo yafuatayo:

**1. Kristo ni Bwana wa sabato.**

Kama Bwana wa sabato, ana mamlaka ya kubadilisha wakati wo wote akitaka.

## NIA YETU

Mungu hapendezwi na yale tunayotenda au fedha tunayotoa tu. Yeye hupendezwa pia na nia zetu ambazo tunatumia na kutoa. Tuhakikishe kwamba tunatoa fedha zilizo sawa, tena tutoe kwa nia safi.

"Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu" (2 Wakorintho 9:7).

"Tena nikitoa mali zangu zote kuwalisha maskini. tena nikijitoa mwili wangu niungue moto, kama sina upendo, hainifaidii kitu" (1 Wakorintho 13:3).



"Kabla haijazaliwa milima, wala hujaiumba dunia, Na tangu milele hata milele ndiwe Mungu" (Zaburi 90:2).

"Bali Bwana atakaa milele" (Zaburi 9:7a).

**2. Mungu ni Roho.**

Maana yake ni kwamba Mungu hana mwili wa nyama, mifupa na damu jinsi tulivyo navyo sisi.

"Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli" (Yohana 4:24).

"Basi Bwana ndiye Roho" (2 Wakorintho 3:17a).

**3. Mungu ni Mwenyezi.**

Hakuna mwisho wa nguvu za Mungu. Hakuna kisichowezekana kwa Mungu.

"Yesu akawakazia macho, akawaambia, Kwa wanadamu hilo haliwezekani; bali kwa Mungu yote yawezekana" (Mathayo 19:26).

"Kwa kuwa hakuna neno lisilowezekana kwa Mungu" (Luka 1:37).

"Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani" (Mathayo 28:18).

**4. Mungu ni Mwenye Kujua Yote.**

Mungu hujua vitu vyote. Hujua kile kilichotendeka na hujua kile kitakachotendeka. Hujua yote tunayofanya na yale tunayofikiri.

"Wala hakuna kiumbe kisichokuwa wazi mbele zake, lakini vitu vyote ni utupu na kufunuliwa machoni pake yeye aliye na mambo yetu" (Waebrania 4:13).

"Kisha wakaomba, wakasema, Wewe, Bwana, ujuaye mioyo ya watu wote" (Matendo 1:24a).

**5. Mungu yuko Kila Mahali.**

Hakuna mahali ambapo mtu anaweza kujificha aepukane na uso wa Mungu.

"Niende wapi nijiepushe na roho yako? Niende wapi niukimbie uso wako? Kama ningepanda mbinguni, Wewe uko; Ningefanya kuzimu kitanda changu, Wewe uko" (Zaburi 139:7-8).

"Macho ya Bwana yako kila mahali; Yakimchunguza mbaya na mwema" (Mithali 15:3).

**6. Mungu Hageuki.**

Mungu yu sawa sikuzote. Vitu vinaweza kubadilika lakini Mungu habadiliki.

"Kwa kuwa mimi, Bwana, sina kigeugeu" (Malaki 3:6a).

"Yesu Kristo ni yeye yule, jana na leo na hata milele" (Waebrania 13:8).

**7. Mungu ni Mtakatifu.**

Mungu huchukia dhambi hujitenga na kilicho na dhambi.

"Wakaitana, kila mmoja na mwenzake, wakisema, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ni Bwana wa majeshi, dunia yote imejaa utukufu wake" (Isaya 6:3).

"Ni nani asiyekucha, Ee, Bwana, na kulitukuza jina lako? kwa kuwa wewe peke yako u Mtakatifu" (Ufunuo 15:4a).

**8. Mungu ni Mwenye Haki.**

Maana yake Mungu huchukia dhambi na kupenda yaliyo mema. Kwa sababu Mungu ni mwenye haki hutaka sisi tutende yaliyo ya haki.

"Bwana ni mwenye haki katika njia zake zote, Na mwenye fadhili juu ya kazi zake zote" (Zaburi 145:17).

"Apate kuonyesha haki yake wakati huu, ili awe mwenye haki na mwenye kumhesabia haki yeye amwaminiye Yesu" (Warumi 3:26).

**9. Mungu ni Mwadilifu.**

Maana yake ni kwamba Mungu anayechukia dhambi na kupenda haki atawahukumu watu wote kwa uadilifu. Watu wengi hufanya uovu ambao hauadhibiwi hapa ulimwenguni. Mungu ataona kuwa haki inatendwa siku ya hukumu.



"Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake; ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja" (1 Wakorintho 16:2).

Jinsi Mkristo atoavyo zaka yake, huwa ni zawadi kwake Yesu Kristo huko mbinguni.

"Na hapa wanadamu wapatikanao na kufa hutwaa sehemu ya kumi; bali huko yeye ashuhudiwaye kwamba yu hai" (Waebrania 7:8).

## WAJIBU WETU

Yesu alifundisha mara nyingi kwa mafumbo juu ya wajibu wa mtumishi kwa bwana wake, na jinsi siku moja, mtumishi huyo atakavyotoa hesabu jinsi alivyomtumikia yule bwana wake. (Soma kwa uangalifu Mathayo 25:14-30.) Siku moja, ni lazima sisi pia kusimama mbele ya Yesu Kristo na kuonyesha jinsi tulivyotumia mali yote ambayo alitukabidhi. Hatutatoa tu hesabu ya fedha zetu lakini ni sehemu tu ya hesabu tutakayotoa.

"Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya"
(2 Wakorintho 5:10).

## MAPENDELEO YETU

Uwakili unapaswa kuchukuliwa kama heshima kuu. Unatupa nafasi ya kushiriki katika kazi ya Ufalme wa Mungu. Tena, kutakuwako na tuzo kwa wale wafanyao uwakili mwema.

"Maana sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu" (1 Wakorintho 3:9).

"Bwana wake akamwambia, Vema, mtumwa mwema na uaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi, ingia katika furaha ya bwana wako" (Mathayo 25:23).

"Na wana wa Lawi, nimewapa zaka yote katika Israeli kuwa urithi wao, badala ya huo utumishi wautumikao, maana, ni huo utumishi wa hema ya kukutana" (Hesabu 18:21).

Pia tunajifunza nia ya Mungu wakati watu walipokataa kutii amri hii.

"Je! mwanadamu atamwibia Mungu? lakini ninyi mnaniibia mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu. Ninyi mmelaaniwa kwa laana, maana mnaniibia mimi, naam, taifa hili lote. Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la" (Malaki 3:8-10).

**2. Jinsi Uwakili ulivyofundishwa na Yesu:**

Kwa hakika Yesu alitoa zaka kwa kuwa alitimiza Sheria.

"Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza" (Mathayo 5:17).

Yesu alidhihirisha kwa kutoa zaka lakini wakati huo huo, aliwakumbusha watu kwamba ni zaidi ya kutoa tu zaka.

"Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki kwa kuwa mnalipa zaka za mnanaa na bizari na jira, lakini mmeacha mambo makuu ya sheria, yaani adili, na rehema, na imani; hayo imewapasa kuyafanya, wala yale mengine msiyaache" (Mathayo 23:23).

**3. Jinsi Uwakili ulifundishwa katika nyaraka:**

Wakristo ni lazima kumsaidia mchungaji ili atumie wakati wake wote katika yale Mungu aliyomwitia.

"Na Bwana vivyo hivyo ameamuru kwamba wale waihubirio Injili wapate riziki kwa hiyo Injili" (1 Wakorintho 9:14).

Inawabidi Wakristo kutoa kufuatana na kadiri ya kufanikiwa kwao na Mungu, kila wakati siku ya kwanza ya juma.



"Mbele za Bwana, kwa maana anakuja, Kwa maana anakuja aihukumu nchi. Atauhukumu ulimwengu kwa haki, Na mataifa kwa uaminifu wake" (Zaburi 96:13).

"Nasi twajua ya kuwa hukumu ya Mungu ni ya kweli juu yao wafanyao hayo" (Warumi 2:2).

**10. Mungu ni Upendo.**

Mungu huwapenda watu wote. Lakini upendo huo haumpofushi Mungu macho asione maasi ya wanadamu. Wala haumzuii kuwaadhibu watu kwa hukumu ya haki wale waliochagua kuishi na kufa katika dhambi yao. Upendo wa Mungu ulimfanya kumtuma Mwanawe pekee, Yesu Kristo, kufia dhambi za ulimwengu wote. Kifo cha Yesu msalabani kwa sababu ya dhambi zetu, kimedhihirisha msamaha wa dhambi na uzima wa milele kwa watu wake. Ili mtu apokee msamaha huo, yambidi kutubu dhambi na kumwamini Kristo kama Mwokozi wake.

"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16).

"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi" (Warumi 5:8).

## SURA YA 3

# BWANA YESU KRISTO

Katika sura hii tutajifunza kweli nne kuhusu Yesu Kristo. Tutaona ya kwamba Biblia inatufundisha kuwa Yesu ni Mwana Mtakatifu wa Mungu. Pia tutajua ya kwamba Yesu alikuwa mwanadamu kama sisi. Hapo tena, tutajifunza kuhusu Yesu kama Mwokozi na Bwana.

## YESU NI MUNGU

Haitoshi kusema kwamba Yesu alikuwa mwalimu mkuu, mbashiri ama mtenda miujiza. Kwa hakika, alikuwa hao wote na kuwazidi pia. Yesu ni Mwana Mtakatifu wa Mungu.

**1. Uungu wake ulidhihirishwa kwa kazi yake ya kuumba.**

"Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika" (Yohana 1:3).

"Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi" (Wakolosai 1:16a).

**2. Uungu wake unaonekana katika yeye na Mungu kuwa ni umoja.**

Yesu ni wa milele kama Mungu alivyo wa milele.

"Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu" (Yohana 1:1).

Katika maandiko hayo, "Neno" limetumika kama jina lingine la Yesu.

Yesu alifundisha ya kuwa yapasa aheshimiwe jinsi Mungu anavyoheshimiwa.

"Ili watu wote wamheshimu Mwana kama vile wanavyomheshimu Baba" (Yohana 5:23a).

Yesu alifundisha kwamba watu wamwamini yeye jinsi wanavyomwamini Mungu.



## SURA YA 9

# UWAKILI

Wakili ni mtu ambaye amepewa kwa imani vitu ambavyo ni mali ya mwingine. Anatazamiwa kulinda na kutumia milki hiyo kwa hali ya kumpendeza mwenyewe. Vitu vyote ni mali ya Mungu. Mali yote tuliyo nayo tumekadhibiwa na Mungu. Inatubidi kutumia mali hiyo na ufahamu kwamba twampendeza Mungu. Uwakili mwema ni kudhihirisha utumishi mwema kwa yale tuliyokabidhiwa na Mungu.

Kwa Mkristo, mali yote, hata maisha yenyewe, ni zawadi kutoka kwa Mungu.

"Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu" (1 Wakorintho 6:19-20).

Mkristo ambaye ni wakili mwema, ni lazima atumie wakati wake, nafsi, mvuto, mali, na vitu vyote kwa utukufu wa Yesu Kristo. Katika somo hili tunahitaji kufikiri zaidi juu ya uwakili wa mali tuliyo nayo.

## UWAKILI KATIKA BIBLIA

**1. Uwakili katika Agano la Kale:**

Tunasoma kwamba mali yote ni ya Mungu.

"Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi" (Mwanzo 1:1).

"Fedha ni mali yangu, na dhahabu ni mali yangu, asema Bwana wa Majeshi" (Hagai 2:8).

Tena tunasoma kwamba Mungu aliamuru watu wake kumtolea zaka (fungu la kumi) kwa kuendesha kazi ya Mungu.

"Tena zaka yote ya nchi, kama ni mbegu ya nchi, au kama ni matunda ya nchi, ni ya Bwana; ni takatifu kwa Bwana" (Mambo ya Walawi 27:30).

vizuri jinsi Yesu alivyoumia katika mwili na jinsi damu yake ilivyomwagika ili tuwe hai.

2. **Chakula cha Bwana hutangazia wote walioko kifo cha Yesu msalabani.**

"Mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo" (1 Wakorintho 11:26). Hakuna fadhili katika kula Chakula cha Bwana bila kuelekeza mawazo yetu kwa Yesu Kristo na kufikiri sana alivyotutendea msalabani Kalvari.

## JINSI YA KULA CHAKULA CHA BWANA

Wakati mwingine swali linaweza kutokea juu ya wakati gani ufaao wa kula Chakula cha Bwana. Biblia haitupi jibu. Lakini ni juu ya kanisa la mahali fulani kuamua ni lini. Inaweza kukumbukwa, mara kwa mara kutosha kuimarisha katika akili na mioyo yetu. Isifanywe mara kwa mara mpaka tuzoee na kukosa kutenda na kushiriki katika ukweli wake.

Usile Chakula cha Bwana bila kufukiri maana yake. Ni lazima kujitayarisha kiroho kabla ya kula.

"Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe. Maana alaye na kunywa, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili" (1 Wakorintho 11:28-29).



"Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi" (Yohana 14:1).

3. **Uungu wake umeonekana kwa kazi zenye nguvu alizozifanya.**

Yesu aliweza kuamuru pepo na bahari wakati wa msukosuko mkuu baharini.

"Mara akaondoka, akazikemea pepo na bahari; kukawa shwari kuu" (Mathayo 8:26b).

Yesu aliamuru pepo wachafu wawatoke watu.

"Yesu akamkemea, akisema, Fumba kinywa, umtoke. Yule pepo mchafu akamtia kifafa, akalia kwa sauti kuu akamtoka" (Marko 1:25-26).

Yesu aliweza kuponya ugonjwa mbaya kwa kusema tu. Katika somo linalofuata tutajifunza jinsi Yesu alivyoweza kumponya mtu aliyekuwa kiwete kwa muda wa miaka 38.

"Yesu akamwambia, Simama, jitwike godoro lako, uende. Mara yule mtu akawa mzima, akajitwika godoro lake, akaenda" (Yohana 5:8-9).

Yesu aliweza kuwafufua wafu. Katika Agano Jipya tunasoma vile Yesu alivyoweza kuwafufua watu watatu waliokuwa wamekufa. Maandiko yanayofuata yatatueleza jinsi mtu mmoja alivyopata kuwa hai baada ya kumaliza siku nne akiwa maiti.

"Naye akiisha kusema hayo, akalia kwa sauti kuu, Lazaro, njoo huku nje. Akatoka nje yule aliyekufa, amefungwa sanda miguuni na uso wake amefungwa leso" (Yohana 11:43-44).

Thibitisho kubwa la Uungu wa Yesu ni kufufuka kwake. Baada ya Yesu kusulibishwa msalabani, alizikwa. Kisha baada ya siku tatu, Yesu alifufuka kutoka katika wafu na akajionyesha mara nyingi kwa wanafunzi wake kabla ya kupaa mbinguni. Maandiko yanayofuata yatatusaidia kufahamu zaidi kusulibiwa kwa Yesu jinsi kunavyohusika na Uungu wake.

"Na kudhihirishwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho ya utakatifu, kwa ufufuo wa wafu, Yesu Kristo Bwana wetu" (Warumi 1:4).

## YESU KAMA MWANADAMU

Hatufundishwi tu kwamba Yesu alikuwa Mwana Mtakatifu wa Mungu bali kwamba alikuwa mwanadamu pia aliyeishi duniani kama wewe na mimi.

**1. Ubinadamu wake ulidhihirishwa kwa kuzaliwa kwake.**

Yesu angeweza kutoka mbinguni akiwa mtu mzima, lakini ilikuwa kupenda kwake kuwa na hali tuliyo nayo sisi. Alizaliwa na mwanamke kama wanadamu wengine wote ili kutimiza jambo hili. Baba yake alikuwa Mungu lakini Yesu aliumbwa tumboni mwa bikira, Mariamu, na kuzaliwa ulimwenguni kama mtoto mchanga.

"Mariamu akamwambia malaika, Litakuwaje neno hili, maana sijui mume? Malaika akajibu akamwambia, Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu" (Luka 1:34-35).

**2. Ubinadamu wake ulitambuliwa kwa ujuzi aliokuwa nao ambao ni sawa na ujuzi wetu sisi.**

Yesu aliweza kuchoka jinsi tunavyochoka.

"Basi Yesu, kwa sababu amechoka kwa safari yake, akaketi vivi hivi kisimani" (Yohana 4:6).

Yesu alihuzunika kupoteza rafiki jinsi sisi tunavyohuzunika.

"Yesu akalia machozi" (Yohana 11:35).

Yesu alikua kama tunavyokua.

"Naye Yesu akazidi kuenea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu" (Luka 2:52).

Yesu alijaribiwa kama tunavyojaribiwa.



nyote katika hiki; kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi" (Mathayo 26:26-28).

## MFANO WA CHAKULA CHA BWANA

Baadhi ya watu wanafundisha kwamba mkate na divai, hasa hugeuka kuwa mwili na damu ya Yesu. Wanasema kuwa mkate na divai si mifano ya mwili na damu ya Yesu bali kwamba vimegeuzwa kabisa kuwa mwili na damu ya Yesu. Kusoma Maandiko Matakatifu kutatufunulia wazi kuwa Yesu alizungumza juu ya mkate na divai kuwa mifano ya mwili wake uliovunjwa na damu yake iliyomwagika. Ebu tusome juu ya chakula cha Bwana katika 1 Wakorintho 11:24-26.

"Naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, Huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu. Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu. Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo" (1 Wakorintho 11:24-26).

Fikiria kwa makini – katika sehemu ya kwanza ya Maandiko, Yesu alizungumza juu ya mkate na divai akisema, "Huu ndio mwili wangu," na "Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu." Ni lazima awe alikuwa akimaanisha kwamba vilikuwa mifano ya vitu hivi kwani baadaye alisema, ". . . maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki. . ." Hivi ni kuonyesha hakuna nafasi ya shaka – vilikuwa vingali mkate na divai. Yesu hakuugeuza mkate kuwa mwili wake wala divai kuwa damu yake. Alivitumia vitu hivyo kama mifano ya mwili wake uliovunjwa na damu yake iliyomwagika.

## KUSUDI LA CHAKULA CHA BWANA

**1. Chakula cha Bwana kinaadhimishwa kwa ukumbusho Wake.**

Yesu alisema: "Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu" (1 Wakorintho 11:24). Tunapokula Chakula cha Bwana inatulazimu kufahamu

mfano wa kuzikwa. Mtu anapozikwa, yeye huwekwa ndani ya kaburi lililochimbwa mchangani. Tunaonyesha mfano huu mtu anapoingizwa ndani ya maji.

Yesu alisema ubatizo unadhihirisha ukweli mkuu – wa mauti ya dhambi kwa aliyeamini katika Kristo, kuzikwa kwa aliyeamini, katika maisha yake ya kale, na ufufuo wa maisha mapya ya aliyeamini katika Kristo. Tunaonyesha hivyo tu tunapomzamisha mwamini ndani ya maji na kumwinua kutoka majini.

## ANAYEPASWA KUBATIZWA

Tukisha kufahamu maana kamili ya ubatizo hakuna shida kujua ni nani anayestahili kubatizwa. Ubatizo huonyesha ufahamu wa kiroho wa mtu na Kristo. Ni hao tu ambao wamekabidhiwa ujuzi huu ndio wanaostahili kuingia maji ya ubatizo. Katika Agano Jipya tunasoma kuhusu wale waliotubu na kumwamini Kristo walibatizwa. Katika amri yake kwetu sisi, Yesu anasema kwamba tuwafanye wanafunzi halafu kuwabatiza.

"Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa" (Matendo 2:41a).

"Ni nani awezaye kukataza maji, hawa wasibatizwe, watu waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi?" (Matendo 10:47).

## CHAKULA CHA BWANA

Agizo la pili ambalo Yesu alitukabidhi ni Chakula cha Bwana. Tunapaswa kuelewa wazi ukweli unaoufuata kuhusu Chakula cha Bwana.

## MWANZO WA CHAKULA CHA BWANA

Yesu mwenyewe alianzisha agizo hili kwa kuwapa wanafunzi wake chakula hicho kabla ya kusulibishwa kwake.

"Nao walipokuwa wakila, Yesu alitwaa mkate, akabariki, akaumega, akawapa wanafunzi wake, akasema, Twaeni, mle; huu ndio mwili wangu. Akakitwaa kikombe, akashukuru, akawapa, akisema, Nyweni



"Bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi" (Waebrania 4:15b).

3. **Ubinadamu wake ulionekana kwa maumivu aliyopata msalabani. Soma juu ya kusulibiwa kwake katika Injili na uhesabu njia nyingine ambazo kwanza Yesu aliteswa mwilini.**

## YESU KAMA MWOKOZI

1. **Kusudi la Yesu kuja ulimwenguni lilikuwa kutuokoa sisi.**

Ni kweli kwamba Yesu alihubiri hotuba nyingi sana za kustaajabisha, kuwafundisha watu juu ya Mungu, na kufanya miujiza mingi alipokuwa anaishi ulimwenguni. Hakukusudia kuja duniani kuyatenda haya tu. Alikuja ili atuokoe kutoka dhambini.

"Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao" (Mathayo 1:21).

"Kama vile Mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi" (Mathayo 20:28).

2. **Yesu ndiye Mwokozi wa pekee.**

Kuna watu wengi wanaodhani kwamba ikiwa mtu ni mwaminifu katika dini yake, mtu huyo kweli ndiye atakayeokolewa. Bali Biblia hutudhihirishia kuwa hakuna wokovu mwingine bila kwa Yesu Kristo.

"Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi" (Yohana 14:6).

"Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo" (Matendo 4:12).

3. **Njia ya Yesu kutuokoa sisi ilikuwa kusulibiwa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu.**

Inatupasa kufahamu kwamba hakuna njia nyingine ya wokovu hasa. Ikiwa mtu alikuwa ataokolewa, ilimpasa Yesu, aliye Mwana wa Mungu asiye na dhambi, kufa badala ya huyo mtu mwenye dhambi.

"Akaendelea mbele kidogo, akaanguka kifulifuli, akaomba, akisema, Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke; walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe" (Mathayo 26:39).

"Na katika Torati karibu vitu vyote husafishwa kwa damu, na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo" (Waebrania 9:22).

"Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu; maana imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti" (Wagalatia 3:13).

"Sisi sote kama kondoo tumepotea; Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; Na Bwana ameweka juu yake Maovu yetu sisi sote" (Isaya 53:6).

## YESU KAMA BWANA

**1. Yesu anazo nguvu zote mbinguni na duniani.**

"Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani" (Mathayo 28:18).

**2. Yesu ni Bwana wa Kila Mkristo.**

"Basi nyumba yote ya Israeli na wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulibisha kuwa Bwana na Kristo" (Matendo 2:36).

"Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka" (Warumi 10:9).

**3. Yesu atajulikana kuwa Bwana na watu wote.**

Ingawa watu wengi wanakana Yesu kuwa Bwana, itatokea siku moja wote watakapokubali kuwa yeye ni Bwana. Iwapo mtu anamkana Yesu anapoishi hapa duniani, naye Yesu atamkana katika siku hiyo.

"Ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi, na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba" (Wafilipi 2:10-11).



## JINSI YA KUBATIZA

Kuna kutoelewana kati ya makanisa kuhusu ubatizo unaostahili. Makanisa mengine humimina maji kichwani. Mengine hunyunyiza maji kidogo kwenye kichwa na mwili wa mtu. Makanisa mengine husema kwamba hakuna haja ya ubatizo. Sisi kama Wabatisti tunasema ubatizo ni muhimu kwa sababu ni tendo ambalo Yesu mwenyewe alituamuru tufanye. Ikiwa tunabatiza, basi tutende katika njia inayotumiwa katika Agano Jipya. Tunazungumzia sababu tatu za kuonyesha kuzamisha kabisa (kuchovya) ndiyo njia ya Maandiko katika ubatizo.

**1. Kuzamisha ni njia ya kweli ya kubatiza kwa sababu ya maana ya neno "batiza."**

Biblia ilipokuwa ikitafsiriwa kutoka lugha ya Kiyunani kwa Kiingereza, neno la Kiyunani *baptidzo* lilitafsiriwa wazi kwa Kiingereza kuwa *baptize*. Tukitaka kuhifadhi maana ya neno hili ni lazima tutumie kamusi ya Kiyunani. Nayo hutwambia kwamba neno *baptidzo* maana yake ni kuweka ndani ya maji, kuchovya, na kuzamisha. Maana ya neno hili hukataza kunyunyiza ama kumimima. Kwa hivyo ni lazima tuzamishe.

**2. Mfano katika Biblia hudhihirisha kwamba kuzamisha ni njia ya kweli ya kubatiza.**

"Ikawa siku zile, Yesu alikuja kutoka Nazareti ya Galilaya, akabatizwa na Yohana katika Yordani. Mara alipopanda kutoka majini, akaona mbingu zinapasuka, na Roho, kama hua, akashuka juu yake" (Marko 1:9-10). (Shika maneno, "alipopanda kutoka majini".)

"Yohana naye alikuwa akibatiza huko Ainoni, karibu na Salimu, kwa sababu huko kulikuwa na maji tele" (Yohana 3:23). (Maji mengi hayana maana sana ikiwa mtu ananyunyiza au anamimina.)

"Akaamuru lile gari lisimame; wakatelemke wote wawili majini, Filipo na yule towashi; naye akambatiza" (Matendo 8:38).

**3. Kuzamisha ni njia kamili ya ubatizo kwa sababu huonyesha kufa, kuzikwa na kufufuka.**

Mwanzoni wa somo letu, tulisema ubatizo ni mfano wa kufa, kuzikwa, na kufufuka. Kunyunyiza na kumimina hakuwezi kuonyesha

**1. Ubatizo ni dhihirisho la utii wa amri ya Yesu Kristo.**

"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu" (Mathayo 28:19).

**2. Ubatizo ni ushuhuda kwa wote wanaotazama. Unawaambia kwamba umekuwa kwa dhambi katika Kristo na kuwa na maisha mapya katika yeye.**

## MAANA YA UBATIZO

1. Kwanza, ni lazima tuelewe wazi kwamba ubatizo ni mfano. Si wokovu, bali unaonyesha mfano au ukweli wa wokovu unaotendeka moyoni mwa aaminiye. Ni lazima tuwe waangalifu kutofananisha mfano na kitu ambacho tunaonyesha kwa mfano. Mtu anaweza kuonyesha picha na kusema, "Huyu ni mama yangu." Sisi sote tunaweza kufahamu kwamba karatasi haikuwa mama yake bali picha ya mama yake. Vivyo hivyo, ubatizo si kifo, kuzikwa na kufufuka bali ni picha ya hayo.

2. Ubatizo hutoa mfano wa kifo, kuzikwa na kufufuka ambavyo mwamini anaona katika moyo wake kwa kumwamini Yesu Kristo.

"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima" (Warumi 6:4).

Kuna maneno matatu muhimu sana katika fungu hili yanayotupasa kuyafikiria kwa ufupi: kifo, kuzikwa, na ufufuo.

Mwamini anapompokea Yesu kuwa Mwokozi, hukubali kifo cha Yesu kama chake mwenyewe juu ya dhambi. Kwa hivyo, amefia dhambi katika Kristo. Ameacha sasa (kama mfu) maisha yake ya kale. Amepokea maisha mapya katika Kristo. Ubatizo ni ishara ya tendo hili la kufa, kuzikwa na kufufuka.



SURA YA 4

# ROHO MTAKATIFU

Siku hizi kuna kutokufahamiana kati ya Wakristo kuhusu hali na kazi ya Roho Mtakatifu. Wengi wetu wamesikia hadithi moja ya vipofu wanne waliosafiri kwenda kujifunza juu ya ndovu. Kila mmoja wao alipapasa sehemu tofauti ya ndovu huyo akafikiri ilifanana na kitu fulani. Baadaye, walipokuwa wakihojiana juu ya ndovu, walianza kubishana sana. Kipofu mmoja aliyepapasa ubavu mmoja wa ndovu alisema alikuwa kama ukuta wa nyumba. Yule aliyeyegusa mguu alifikiri kwamba ni kama mti. Wa tatu aliyeshika mkia alikaza kuwa ndovu ni kama kamba. Wa mwisho aliyeshika mkonga wa ndovu huyo, aliamini kwamba alikuwa kama nyoka kubwa. Hapo tunaona wazi kuwa kutofahamiana kulitokea kwa sababu kila mtu alishika sehemu tofauti na mwenzake.

Kutokuelewa juu ya Roho Mtakatifu hutokea katika njia ya namna hiyo. Maandiko yanapotufundisha kuhusu sehemu moja ya tabia ya Roho Mtakatifu au huduma yake na mengine yote huachwa, basi mabishano hutokea. Itakuwa shida kuweka pamoja Maandiko yote juu ya Roho Mtakatifu katika somo hili. Tumejaribu, hata hivyo, kuchagua Maandiko yatakayotupa fahamu njema na huduma ya Roho Mtakatifu.

## UUNGU WA ROHO MTAKATIFU

Katika somo letu juu ya Utatu (Sura ya 2) tulijifunza kwamba Roho Mtakatifu ni umoja na Mungu Baba na Mungu Mwana. Jifunze tena kwa makini Maandiko hayo. Hapo tunaona kwamba Roho Mtakatifu ni Mungu. Roho Mtakatifu haonekani, ni Mtakatifu, Mwenye uweza wote, aliye kila mahali wakati mmoja, na ni ufunuo wa kiroho wa Mungu mwenyewe. Biblia hutufundisha kwamba ni katika Roho Mtakatifu ambamo Mungu na Yesu huishi ndani ya Mkristo na kuwa naye siku zote.

## NAFSI YA ROHO MTAKATIFU

Tusidhani Roho Mtakatifu kuwa ni "kitu", Roho Mtakatifu ni mtu. Katika Biblia tunaona ya kwamba mtu anaweza kumwasi, kumwambia uongo, na kumhuzunisha Roho Mtakatifu. Hatuwezi kuasi kuambia uongo ama kuhuzunisha "Kitu" – bali mtu pekee.

"Lakini wakaasi, wakamhuzunisha Roho yake Mtakatifu" (Isaya 63:10).

"Kwa sababu hiyo nawaambia, Kila dhambi na kila neno la kufuru watasamehewa wanadamu, ila kwa kumkufuru Roho hawatasamehewa" (Mathayo 12:31).

"Petro akasema, Anania, kwa nini Shetani amekujaza moyo wako kumwambia uongo Roho Mtakatifu, na kuzuia kwa siri sehemu ya thamani ya kiwanja?" (Matendo 5:3).

"Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi" (Waefeso 4:30).

## KAZI YA ROHO MTAKATIFU

Kujifunza Agano la Kale kutafunua upesi kwamba Roho Mtakatifu alifanya kazi katika maisha ya wanadamu kabla ya kuja kwake Yesu ulimwenguni. Mungu aliwapa watu fulani Roho Mtakatifu kuwawezesha kutimiza utumishi. Soma habari za Gidioni (Waamuzi 6:34) Samsoni (Waamuzi 14:6) Daudi (1 Samueli 16:13). Tunaona ya kwamba watu hawa walipewa Roho wa Mungu kwa kusudi halisi – kumtumikia Mungu.

Tena, tukijifunza juu ya maisha ya Yesu, twaona kwamba Roho wa Mungu aliteremka kutoka mbinguni kama hua baada ya Yesu kubatizwa na kutua juu yake. Yohana alisema, "Tena Yohana akashuhudia akisema, Nimemwona Roho akishuka kama hua kutoka mbinguni; naye akakaa juu yake" (Yohana 1:32). Yesu mwenyewe alifundisha ya kwamba kazi zote alizofanya zilifanywa na Roho Mtakatifu wa Mungu. "Lakini mimi nikitoa pepo kwa Roho wa Mungu, basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia" (Mathayo 12:28).





# MAAGANO YA KANISA

Tunapojifunza Agano Jipya tunaona ya kwamba Yesu alitoa maagizo mawili ya kufuatwa. Kila mojawapo ya maagizo haya linafundisha ukweli mkubwa wa Injili. Maisha ya kiroho ya makanisa yetu yatahuishwa zaidi kwa njia ya ufahamu mwema na uchunguzi wa maagizo haya mawili. Fbu tufikirie kwanza agizo la ubatizo.

## UBATIZO

### UBATIZO HAUOKOI

Watu wanaoelewa vibaya Maandiko wanaamini kwamba ubatizo ni wa lazima ili mtu apate kuokolewa. Lazima tuelewe vizuri kwamba ubatizo hauokoi.

1. **Ubatizo hauokoi, kwa sababu maji hayasafishi dhambi – bali damu ya Yesu Kristo ndiyo inayoweza kuondoa.**

"... na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote" (1 Yohana 1:7).

2. **Ubatizo hauokoi kwa sababu ni kitendo cha mtu, lakini wokovu ni kipawa cha Mungu.**

"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu" (Waefeso 2:8-9).

3. **Tunafahamu kwamba ubatizo hauokoi kwa sababu mwizi aliyeangikwa msalabani aliokolewa kwa neema ya Mungu bila kubatizwa.**

"Yesu akamwambia, Amini, nakuambia, leo hivi utakuwa pamoja nami peponi" (Luka 23:43).

## UMUHIMU WA UBATIZO

Wako watu wengine watakaosema, "Kwa kweli, ikiwa ubatizo hauokoi, kwa nini tupate taabu ya kubatizwa?" Ingawa ubatizo hauokoi, ni muhimu.

"Kwa maana sikujiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu" (Matendo 20:27).

**4. Ibada, Kujengana, na Ushirika.**

"Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali" (Matendo 2:42).

"Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile inakaribia" (Waebrania 10:24-25).

"Hilo tuliloliona na kulisikia, twawahubiri na ninyi; ila nanyi pia mpate kushirikiana nasi; na ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwana wake Yesu Kristo" (1 Yohana 1:3).



Walakini, katika Somo hili, tunahusika hasa na kazi ya Roho Mtakatifu katika maisha ya wanadamu siku hizi. Kuna Maandiko ambayo yameeleza vizuri sana kazi ya Roho Mtakatifu kuliko mwingine yote. Matendo yake mengine yote ni sehemu ya kazi hii kubwa. Katika Yohana 16:14 tunasoma maneno ya Yesu alivyoyaeleza jinsi Roho Mtakatifu atakavyokuwa, "Yeye atanitukuza mimi." Kifungu hicho kinaweza kutumiwa kama kipimo cha mambo mengi ambayo watu hutumaini kufanya kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Ikiwa Yesu hakutukuzwa katika jambo, basi halikutendeka kwa uwezo wa Roho wa Mungu.

Wakati tunapofikiri habari ya kazi ya Roho Mtakatifu, inatupasa kufikiri juu yake katika njia mbili muhimu; (1) Kazi ya Roho Mtakatifu katika moyo wa mtu aliyepotea, na (2) Kazi ya Roho Mtakatifu katika maisha ya Mkristo.

**1. Kazi ya Roho Mtakatifu katika moyo wa mtu ambaye hajaokoka:**

Kuna andiko moja linalotwambia zaidi juu ya kazi ambayo Roho Mtakatifu anaifanya katika moyo wa mtu ambaye hajaokoka. "Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu. Kwa habari ya dhambi, kwa sababu hawaniamini mimi; kwa habari ya haki, kwa sababu mimi naenda zangu kwa Baba, wala hamnioni tena; kwa bahari ya hukumu, kwa sababu yule mkuu wa ulimwengu huu amekwisha kuhukumiwa" (Yohana 16:8-11).

Wakati mtu ambaye hajaokoka anapotambua kwamba yu mwenye dhambi, na kuwa Yesu ndiye mwenye haki, na kuwa atahukumiwa kwa ajili ye dhambi zake, hii huwa ni kazi ya Roho Mtakatifu katika moyo wake.

**2. Kazi ya Roho Mtakatifu katika maisha ya Mkristo:**

Kuna kazi nyingi ambazo Roho Mtakatifu hufanya katika maisha ya Mkristo. Katika somo hili tutafikiria baadhi ya kazi saba anazofanya.

**(1) Roho Mtakatifu ni mwenye kutoa maisha mapya.**

"Lakini, ikiwa Roho wake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu ataihuisha na

miili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu" (Warumi 8:11).

**(2) Roho Mtakatifu ni Mfariji wetu.**

"Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele" (Yohana 14:16).

**(3) Roho Mtakatifu ni Mwalimu wetu.**

"Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia" (Yohana 14:26).

**(4) Roho Mtakatifu hufanya kuwa na uzao mwema katika maisha ya Kikristo.**

"Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi. . ." (Wagalatia 5:22-23).

**(5) Roho Mtakatifu hutupa nguvu katika utumishi.**

"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi" (Matendo 1:8).

**(6) Roho Mtakatifu hutuongoza tufanyapo kazi ya Mungu.**

"Basi hawa walipokuwa wakimfanyia Bwana ibada na kufunga, Roho Mtakatifu akasema, Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliyowaitia" (Matendo 13:2).

"Wakapita katika nchi ya Frigia na Galatia, wakikatazwa na Roho Mtakatifu, wasilihubiri lile neno katika Asia" (Matendo 16:6).

**(7) Roho Mtakatifu ni mpaji wa vipawa vya kiroho.**

"Lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye"
(1 Wakorintho 12:11).

Kuna habari nyingine zinazotakiwa kujulikana vizuri. Hupatikana katika sura ya 12, 13 na 14 ya 1 Wakorintho ukiisoma kwa makini.

A. Vipawa vya kiroho hupeanwa na Roho Mtakatifu lakini vipawa tofauti hupewa watu mbalimbali. Kwa sababu mtu mmoja hapewi



"Ndugu, twawaagiza katika jina la Bwana Yesu Kristo, jitengeni nafsi zenu na kila ndugu aendaye bila utaratibu, wala si kwa kufuata mapokeo mliyoyapokea kwetu" (2 Wathesalonike 3:6).

"Kumtolea Shetani mtu huyo, ili mwili uadhibiwe" (1 Wakorintho 5:4-5).

2. **Ni lazima liweko kusudi na nia halisi wakati kanisa linapomwadilisha mtu.**

"Ili na roho iokolewe katika siku ya Bwana Yesu" (1 Wakorintho 5:5).

Maadili yanapoanza kuwa ni ya lazima, ni lazima kufanywa na kanisa katika njia ya roho ya upendo. Yasitimizwe kwa roho ya kulipiza kisasi ama kuadhibu, bali na matumaini kwamba mwenye dhambi ataweza kuziona dhambi zake, atubu na kurudia kumfuata Bwana Yesu.

## KAZI YA KANISA

1. **Kuwatafuta waliopotea ili wamwamini Kristo kwa njia ya kuhubiri Injili.**

"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu" (Mathayo 28:19).

"Na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu" (Luka 24:47).

"Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye" (Warumi 1:16).

2. **Kuwabatiza waliookoka.**

"Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu" (Mathayo 28:19).

"Nao walioliipokea neno lake wakabatizwa" (Matendo 2:41).

3. **Kufundisha kwa ukamilifu njia ya Ukristo.**

"Na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi" (Mathayo 28:20).

Wakristo walipopatwa na tatizo kubwa, ilikuwa kazi ya kanisa lote kuamua yaliyofaa kutendwa.

"Basi ikawapendeza mitume na wazee na kanisa lote kuwachagua watu miongoni mwao na kuwapeleka Antiokia pamoja na Paulo na Barnaba" (Matendo 15:22).

Wakati jambo lilipotokea na kuleta maadili ya kanisa, ilikuwa kazi ya kanisa lote kuadhibu yule aliyekosa miongoni mwao. Angalia 1 Wakorintho 5:1-5.

## VIONGOZI WA KANISA

**1. Mchungaji.**

Maneno haya mchungaji, mzee, na askofu yana maana moja katika Agano Jipya. Katika Matendo sura ya 20, Paulo aliwaita wazee wa kanisa la Efeso (kifungu cha 17). Katika kifungu cha 28 huwaambia kuwa Roho Mtakatifu amewafanya waangalizi (Maskofu), na kwamba kazi yao ni kulilisha (chunga) kanisa. 1 Petro 5:1

Labda swali linaweza kutokea kwamba, "Ni nani anayeweza kuwa mchungaji wa kanisa?" Tunaweza kupata ushuhuda wa Mungu katika kitabu cha 1 Timotheo 3:1-7 na Tito 1:7-9. Vifungu hivyo vyote visomwe na kila mmoja katika kanisa. Kanisa linapaswa kukumbuka kuwa Mungu naye alikuwa na sababu ya kutoa sifa hizo. Kanisa linapomtafuta mchungaji, linapaswa kuhakikisha kwamba mtu huyo ana sifa hizo kabla hajakaribishwa kuwa mchungaji wa kanisa.

**2. Mashemasi.**

Makanisa ya Agano Jipya yalikuwa na Mashemasi pia. Tabia ya mashemasi inapatikana katika 1 Timotheo 3:8-13.

## KUWAADILISHA WASHIRIKI

**1. Mara kwa mara ni lazima kumwadilisha mshiriki.**

Wakati maisha ya mshiriki wa kanisa yanapoonekana kuwa kinyume cha mafundisho ya Yesu na kwamba analeta aibu kanisani na mafarakano katika mambo ya Kristo, inakuwa msaada kwa kanisa kumwadilisha.



sawa na mwenzake si kusema ya kuwa yeye si Mkristo kama mwenzake.

B. Vipawa vyote vya Roho Mtakatifu vitakuwa vya kuleta kusudi la kumtukuza Yesu Kristo, hii ni kazi ya Roho Mtakatifu. Soma tena Yohana 16:14.

C. Kipawa cha ndimi huhesabiwa kuwa kisicho cha maana sana.

D. Mkristo hushurutishwa kutafuta vipawa vilivyo bora. Kilicho cha maana katika hivyo vyote ni "Upendo." (Soma 1 Wakorintho 13:1-13.) Kingine ni kile cha unabii (kuhubiri) (Soma 1 Wakorintho 14:1, 39).

E. Iwapo mtu awaye yote anahitaji kunena kwa lugha katika kanisa, ziko amri mahsusi zinazombidi kufuata:

Si zaidi ya watu wawili au watatu kunena. 1 Wakorintho 14:27.

Waruhusiwe kunena mmoja baada ya mwingine, si wote pamoja. 1 Wakorintho 14:27.

Wasiruhusiwe kunena bila mtu kutafsiri. 1 Wakorintho 14:27-28

Yale yanayosemwa lazima yawe ya kumtukuza Yesu Kristo na ya kujenga kanisa. Yohana 16:14; na 1 Wakorintho 14:26.

## KUISHI NDANI KWA ROHO MTAKATIFU

Biblia hutufundisha kwamba Roho Mtakatifu huishi ndani ya moyo wa kila Mkristo wa kweli. Mtu anapozaliwa tena, Roho wa Mungu huingia ndani ya moyo wake. Ikiwa mtu hana Roho Mtakatifu ndani ya moyo wake, yeye si Mkristo.

"Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake" (Warumi 8:9).

"Ili kwamba baraka ya Ibrahimu iwafikilie Mataifa katika Yesu Kristo, tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani" (Wagalatia 3:14).

## KUJAZWA ROHO MTAKATIFU

Kuna tofauti kubwa kati Roho Mtakatifu kuishi ndani ya moyo wa mtu na moyo wa Mkristo kujazwa au kumilikiwa kabisa na Roho Mtakatifu. Mungu anataka tumtegemee ndipo tujazwe na Roho wake Mtakatifu na kutawala maisha yetu yote. Hapo ndipo Mungu anaweza kututumia katika njia bora ya kumtumikia Bwana na Mwokozi wetu, Yesu Kristo.

"Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho" (Waefeso 5:18).

"Hata walipokwisha kumwomba Mungu, mahali pale walipokusanyika pakatikiswa, wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri" (Matendo 4:31).

Mungu yuko tayari na tena ana hamu kujaza kila moyo Roho wake. Walakini, kabla hili halijaweza kutendeka, ni lazima kwanza tuondoe mioyoni mwetu vile vitu vinavyomhuzunisha Mungu. Ni lazima kutii uongozi wa Roho Mtakatifu katika kila jambo. Baada ya kuwa tayari, tutaona ukuu wake katika maisha yetu kwa njia ambayo haijajulikana kamwe kwetu.



**2. Kanisa lapaswa kuwa na washiriki waliobatizwa kulingana na Maandiko. (Soma sura inayoeleza "Maagizo ya kanisa" kwa majadiliano zaidi.)**

"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu" (Mathayo 28:19).

"Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu" (Matendo 2:41).

Kulingana na Maandiko hayo na mengine mengi, tunajifunza kwamba Yesu aliamuru ubatizo, na kwamba makanisa ya Agano Jipya yatumie ubatizo. Ndipo sasa tunasema kwamba washiriki wa makanisa wapokee ubatizo wa Agano Jipya.

## UTAWALA WA KANISA

Sisi kama Wabatisti tunaamini na kufuata uhuru wa kujitawala wenyewe katika kanisa. Msingi wa imani na desturi hii umo katika mambo yafuatayo:

**1. Uongozi wa Yesu Kristo.**

Tumekwisha ona katika sura hii ya kuwa Kristo ndiye kichwa cha kanisa. Yeye ndiye kichwa cha kanisa kama vile kichwa kilivyo kwa mwili. Ni kichwa ambacho huongoza kila kiungo cha mwili. Vivyo hivyo, Kristo katika Roho Mtakatifu ndiye anayemwongoza kila Mkristo na pia kuongoza kundi zima.

**2. Usawa wa Waamini wote.**

Biblia inafundisha kuwa sote tu sehemu za mwili. Hakuna kiungo cha mwili kinachoweza kutawala kingine. Mkono hauwezi kuuambia mguu jinsi ya kufanya – hii ni kazi ya kichwa. Jifunze kwa makini Warumi 12:3-6 na 1 Wakorintho 12:14-20.

**3. Mifano inayoonekana katika Agano Jipya.**

Mashemasi walipochaguliwa, ilifanywa na kanisa nzima. Soma Matendo 6:1-6.

Wakristo walipopatwa na tatizo kubwa, ilikuwa kazi ya kanisa lote kuamua yaliyofaa kutendwa.

"Haya uyaonayo uyaandike katika chuo, ukayapeleke kwa hayo makanisa saba" (Ufunuo 1:11).

Tunapojifunza kuhusu kanisa katika sura hii, tutafikiria habari za kundi maalum, linaloonekana, na kusanyiko la waamini. Itatupasa kuhakikisha ya kuwa tabia ya makanisa ya Agano Jipya itakuwa tabia ya kanisa letu.

## KICHWA CHA KANISA

Hakuna mtu wala watu wanaoweza kuwa kichwa cha kanisa la Agano Jipya. Yesu Kristo pekee ndiye kichwa cha kanisa. Mtu ye yote anayetafuta kuwa kichwa katika kanisa yeye hutaka kupokea nafasi ambayo ni ya Yesu Kristo.

"Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa" (Waefeso 1:22).

Sisi ni washiriki wa kanisa kama vile viungo vingi katika mwili mmoja vilivyo. Yesu Kristo ni kichwa cha kanisa.

## USHIRIKA WA KANISA

Katika Agano Jipya tunaona ya kwamba kuna masharti mawili yaliyotolewa ndipo uwe mshiriki wa kanisa: Wokovu na Ubatizo.

**1. Kanisa lapaswa kuwa na watu waliookoka katika ushirika wake.**

"Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa" (Matendo 2:47).

"Kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho, wale waliotakaswa katika Kristo Yesu" (1 Wakorintho 1:2).

Ni dhahiri kwamba wakati mwingine watu ambao hawajaokoka huwa washiriki wa kanisa fulani. Huwa hivyo kwa mapenzi ya binadamu, lakini ni kinyume cha mpango wa Mungu. Watu wengine huwa washiriki wa kanisa kwa ungamo lisilo la haki. Makanisa mengine yanawaleta watoto wachanga katika ushirika wa makanisa yao. Mungu hutaka wanaozaliwa mara ya pili tu katika ushirika wa kanisa.



SURA YA 5

# DHAMBI NA SHETANI

Yako maswali mengi yanayoulizwa juu ya Shetani na hayawezi kujibiwa kwa sababu Mungu hakuamua kutuambia majibu katika Biblia. Hata hivyo, ya kutosha yamekwisha kufunuliwa kujibu maswali mengine ya kawaida. Biblia hutufundisha ya kutosha ili tuweze kufahamu vyema asili ya adui yetu wa kiroho, Shetani. Ebu tufikirie baadhi ya maswali mengine ambayo huulizwa mara kwa mara kuhusu Shetani.

**1. Shetani alitoka wapi?**

Biblia inafundisha wazi kwamba Mungu aliviumba vitu vyote. Kwa kuwa ni kweli, basi Shetani aliumbwa na Mungu.

**2. Je, Mungu alimwumba Shetani kuwa mwovu kama alivyo sasa?**

Jibu ni, La. Mungu kila wakati anatenda kufuatana na asili yake. Ni kinyume na asili (ama tabia) ya Mungu kuumba kilicho kibaya. Ebu tuangalie ulimwengu wetu kuwa kama mfano. Kuna maasi mengi katika ulimwengu wa sasa. Haikuwa kweli hivyo tangu Mungu alipoanza kuumba ulimwengu. "Mungu akaona kila kitu alichokifanya, na tazama, ni chema sana" (Mwanzo 1:31). Tunafahamu mara kwamba ulimwengu wa siku hizi si kama Mungu alivyouumba – mabadiliko yametokea. Ndivyo ilivyokuwa kwa Shetani. Yeye ni mwovu sasa, ingawa Mungu hakumuumba jinsi alivyo. Tukisoma Agano Jipya, inaonekana kuwa Shetani alikuwa malaika ambaye aliasi mbele za Mungu na akatupwa kutoka mbinguni. Soma vifungu vinavyofuata kwa uangalifu:

"Kwa maana ikiwe Mungu hakuwaachilia malaika waliokosa, bali aliwatupa shimoni, akawatia katika vifungo vya giza, walindwe hata ije hukumu." (2 Petro 2:4)

"Na malaika wasioilinda enzi yao wenyewe, lakini wakayaacha makao yao yaliyowahusu, amewaweka katika vifungo vya milele chini ya giza kwa hukumu ya siku ile kuu" (Yuda 1:6).

"Akawaambia, Nilimwona Shetani, akianguka kutoka mbinguni kama umeme" (Luka 10:18).

**3. Kazi ya Shetani ni ipi?**

Jina lake linamaanisha adui. Ni adui wa Mungu na wote wanaomfuata Mungu. Hujaribu, kuwadanganya, na kutafuta kuwavuta wengine kwenda jehanam pamoja naye.

**4. Mwisho wake utakuwa nini?**

Adhabu ya milele katika jehanam ndio utakaokuwa mwisho wa Shetani pamoja na wale wanaomfuata.

"Na yule Ibilisi, mwenye kuwadanganya, akatupwa katika ziwa la moto na kiberiti" (Ufunuo 20:10).

"Kisha atawaambia na wale walioko mkono wake wa kushoto, Ondokeni kwangu mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake" (Mathayo 25:41).

## MWANZO WA DHAMBI

Kabla ya kujifunza habari kuhusu mwanzo wa dhambi, inatupasa kutafuta jibu la swali linaloulizwa mara kwa mara. Kwa nini Mungu mwenyezi anayechukia dhambi aliruhusu dhambi kuingia ulimwenguni? Jibu lake ni dhahiri. Ikiwa Mungu angemwumba mtu mwenye upendo wa kweli na utii, mtu huyo angepata njia ya kumchukia na kutokumtii Mungu. Fikiria habari kwa njia hii. Tuseme unao wana wawili unaowapenda sana. Unataka wana hao wakupende na kukutii. Fikiria kwamba siku moja unatarajia kwenda safari. Safari hiyo ni ya siku nzima. Lakini unafahamu vyema kwamba si vizuri watoto wako kucheza mwituni. Kwa hivyo, uliwaita wote na kuwaambia, "Sitakuwepo siku nzima. Chezeni katika sehemu hii iliyo wazi karibu na nyumba. Msicheze huko mwituni." Kisha ukamfunga mtoto mmoja kwenye mti. Mtoto huyo hangeweza kutoroka na kwenda kucheza mwituni. Mtoto wa pili alipewa uhuru wa kucheza na kutembea apendavyo.

Watoto wote waliamriwa kubaki kwenye kiwanja. Mmoja hangeweza kuasi na yule mwingine angeweza. Aliporudi baada ya siku kumalizika, aligundua ya kuwa watoto wote walishinda nyumbani. Kwa kweli





# KANISA

Wakati mjenzi anapojenga nyumba, ni lazima aifuate ramani iliyochorwa. Mungu ametupa mpango wake katika Agano Jipya. Kwa hivyo, ni lazima tuifuate mpango wake kwa uangalifu katika kuyajenga makanisa yake ambayo yatampendeza Mungu.

Neno "kanisa" limetumiwa mara 114 katika Agano Jipya. Neno hili limetumiwa kuzungumzia kundi la Wakristo wanaoishi na kuabudu katika sehemu fulani. Walakini, kuna mara chache wakati neno hili linapotumika kuonyesha waamini wote, waliozaliwa mara ya pili kama kundi moja. Linapotumiwa katika njia hii, linafundisha ukweli kwamba waamini wote waliozaliwa tena wameungana kiroho pamoja na Kristo, jinsi viungo vingi vya mwili vinavyoungana na kichwa. Wakati neno "kanisa" linapotumiwa hivi, mara nyingi tunalifananisha na "Kanisa la Ulimwengu wote" ama Kanisa lisiloonekana. Kulingana na Maandiko yafuatayo, twaweza kuona likitumiwa kwa njia hii.

"Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa; naye ni mwokozi wa mwili" (Waefeso 5:23).

"Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa" (Wakolosai 1:18).

Ukisoma Maandiko kwa uangalifu utaona yanadhihirisha wazi karibu kila sehemu ambapo neno "kanisa" linatumiwa, linalinganishwa na kundi fulani la Wakristo.

"Na huko Antiokia katika kanisa lililokuwapo palikuwa na manabii na waalimu" (Matendo 13:1).

"Toka Mileto Paulo akatuma watu kwenda Efeso, akawaita wazee wa kanisa" (Matendo 20:17).

"Nisalimieni na kanisa lililomo katika nyumba yao" (Warumi 16:4).

"Kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho" (1 Wakorintho 1:2).

5. **Aliyeamini analindwa na nguvu za Mungu, ili akisha kuokolewa asipotee kamwe.**

"Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mpate wokovu ulio tayari kufunuliwa wakati wa mwisho" (1 Petro 1:5).

"Kondoo wangu waisikia sauti yangu; nami nawajua. nao wanifuata. Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu" (Yohana 10:27-28).



mmoja hakuasi kwa sababu alifungwa mtini. Na mwingine alionyesha upendo na utii wake kushinda hapo nyumbani ingawa angaliweza kwenda. Tunaweza kusema yule mtoto angeweza kuasi lakini akachagua kutii alidhibitisha utumishi wake mwema kwako.

Mungu hakuweka nafasi ya dhambi katika bustani na kumpa mwanadamu hiari ya kuchagua ili aweze kuasi. Alifanya hivyo ili mwanadamu aweze kuthibitisha upendo na upole kwake. Wakati mwanadamu alipoasi, dhambi iliingia duniani.

Soma kwa uangalifu Mwanzo 2:8 hadi Mwanzo 3:24. Andiko hili linalohusika na dhambi ya kwanza, linatuongoza kufahamu mengi juu ya dhambi. Tunajifunza ukweli ufuatao kwalo:

1. Mungu aliandaa vyote vilivyokuwa vyema vya kufaidi mwanadamu.
2. Mungu alimkataza mwanadamu kilicho kibaya tu.
3. Shetani, katika hali ya nyoka, alitokea na kumjaribu Hawa. Alitaka Hawa kuamini Mungu alimficha kitu fulani kizuri. Tena akamhakikishia Hawa kwamba Mungu hatamwadhibu kwa kifo ikiwa ataghairi kumtii.
4. Hawa alikata shauri kuvunja mapenzi ya Mungu na kula tunda alilokatazwa. Kisha akampatia Adamu naye akala tunda hilo pia.

## MAANA YA DHAMBI

Katika mambo tuliyoyaona hapo juu, tunataka kujifunza hasa maana ya dhambi. Dhambi ni wakati mtu anapokataa mapenzi ya Mungu na kufanya mapenzi yake mwenyewe. Hivyo ndivyo Adamu na Hawa walivyofanya. Walifahamu mapenzi ya Mungu lakini wakachagua kuyakataa ili waweze kutenda yale waliyopenda wenyewe.

## KUWAKO KWA DHAMBI KILA MAHALI

Mungu anatufundisha katika Neno lake ya kwamba kila mtu po pote alipo amefanya dhambi mbele yake. Kulingana na maoni ya mwanadamu, tunaonekana kuwa wakamilifu. Lakini Mungu hahukumu

vile anavyohukumu mwanadamu, Mungu hutulinganisha na wema wake mwenyewe. Anapofanya hivi, husema wote wamefanya dhambi.

"Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu" (Warumi 3:23).

"Sisi sote kama kondoo tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe" (Isaya 53:6).

"Kwa maana sisi sote tumekuwa kama mtu aliye mchafu, na matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi" (Isaya 64:6a).

"Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo, mwetu" (1 Yohana 1:8).

"Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi" (Yakobo 4:17).

## MATOKEO YA DHAMBI

Hatuwezi kuyataja maasi yote ambayo yameingia ulimwenguni kama tokeo la dhambi. Maneno hayawezi kusimulia huzuni na maumivu yaliyoletwa na dhambi. Tukiangalia ulimwengu wa siku hizi kuna dhiki, mauti, uwongo, chuki, vita, udhaifu, ugonjwa, njaa, na umaskini, na ni lazima tukumbuke kwamba Mungu hakukuumba jinsi ulivyo. Ulimwengu haukutokea hivi mpaka dhambi ilipoingia. Hasa twataka kuonyesha njia mbili ambazo kwanza dhambi ilimdhuru mwanadamu.

**1. Dhambi huharibu ushirika wetu na Mungu.**

Dhambi ilipopata nafasi katika mioyo ya Adamu na Hawa, walijiona wenye hatia. Waliuficha uchi wao na kujificha ili wasionekane na Mungu. Dhambi hiyo iliwafanya wafukuzwe kutoka Bustani ya Edeni na mbele ya uso wa Mungu. Sasa, kama wakati huo, dhambi ingali ikitutenganisha na Mungu.

"Lakini maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu, na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone, hata hataki kusikia" (Isaya 59:2).



## MATOKEO YA WOKOVU

**1. Mwamini husafishwa na husamehewa dhambi zote.**

"Haya, njooni, tusemezane, asema Bwana. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu". (Isaya 1:18).

"Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake" (Ufunuo 1:5b).

**2. Mwamini anakuwa kiumbe kipya kwa Roho wa Mungu anayeishi ndani yake. Wakati huo yeye hupenda kufanya mapenzi ya Mungu.**

"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazama! yamekuwa mapya" (2 Wakorintho 5:17).

"Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake" (Warumi 8:9).

**3. Mwamini huamini kwa sababu Roho wa Mungu anaishi ndani yake, atamtumikia Mungu badala ya Shetani.**

"Na jinsi mlivyomgeukia Mungu mkaziacha sanamu, ili kumtumikia Mungu aliye hai, wa kweli" (1 Wathesalonike 1:9).

"Maana sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu" (1 Wakorintho 3:9a).

**4. Mwamini ana nyumba ya milele mbinguni inayomngojea yeye.**

"Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali" (Yohana 14:2).

"Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele" (1 Wathesalonike 4:16).

“Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti; ili, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa” (1 Petro 2:24).

**3. Wokovu huu unapatikana kwa toba na imani.**

Toba ni mabadiliko ya moyo yanayoonyesha mabadiliko ya vitendo. Toba ya kweli huhusiana na mambo matatu; ujuzi kwamba mtu amemtendea Mungu dhambi; huzuni ya kweli kwa sababu ya dhambi; na kuacha dhambi kabisa. Mungu hufundisha wazi katika Neno lake kwamba ni lazima mtu atubu kwanza kabla hajapokea wokovu.

“Tokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri, na kusema, Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia” (Mathayo 4:17).

“Nawaambia, Sivyo; lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo” (Luka 13:3).

“Nikiwashuhudia Wayahudi na Wayunani wamtubie Mungu, na kumwamini Bwana wetu Yesu Kristo” (Matendo 20:21).

Imani ni mvuto unao kufanya uyatoe maisha yako kwa ajili ya kitu unachoamini. Kumwamini Yesu Kristo ni imani inayomfanya mtu atoe maisha yake kwa Yesu. Wokovu unapatikana wakati Imani kama hiyo inapowekwa katika Yesu kama Mwokozi na Bwana.

“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele” (Yohana 3:16).

“Wakamwambia, Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako” (Matendo 16:31).

“Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu” (Waefeso 2:8).

“Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na tuwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo” (Warumi 5:1).



“Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti” (Warumi 6:23a).

“Mauti na Kuzimu zikatupwa katika lile ziwa la moto. Hii ndiyo mauti ya pili, yaani hili ziwa la moto. Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto” (Ufunuo 20:14-15).

“Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili” (Ufunuo 21:8).

“Kisha atawaambia na wale walioko mkono wake wa kushoto, Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake” (Mathayo 25:41).

Wanadamu wanaweza kudharau na kucheka dhambi, bali Mungu hataweza. Mungu huona na kuihukumu dhambi. Kwa hivyo sisi sote tumetenda dhambi na hatuna la kufanya ili tuepuke ghadhabu tuliyowekewa. Lakini Mungu, katika mapenzi yake kwetu ametengeneza njia ambayo dhambi zetu zitaadhibiwa na sisi tuweze kuokolewa. Jifunze kwa uangalifu sura ifuatayo juu ya wokovu.

## SURA YA 6

# WOKOVU

Katika somo lililopita tulijifunza kwamba wote wamefanya dhambi na wanakaa chini ya hukumu ya Mungu. Katika sura hii twataka kujifunza njia ya wokovu ambayo Mungu ametoa bure kwa watu wote kwa njia ya Mwanawe, Yesu Kristo. Yatupasa kwanza kuelewa neno hili:

## MWANADAMU HAJIOKOI MWENYEWE

Ebu tuangalie sababu nne zinazomfanya mtu asiweze kujiokoa mwenyewe.

**1. Mtu hawezi kujiokoa mwenyewc kwa sababu wema alionao hauwezi kufikia wema unaoweza kupendeza machoni pa Mungu.**

"Kwa maana sisi sote tumekuwa kama mtu aliye mchafu, na matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi" (Isaya 64:6).

**2. Mtu hawezi kujiokoa mwenyewe kwa sababu Mungu anatwambia kwamba hakuna mtu atakayeokolewa kwa njia ya matendo yake mwenyewe.**

"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu, wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu" (Waefeso 2:8-9).

**3. Mtu hawezi kujiokoa mwenyewe kwa sababu ni lazima apate mshahara wa dhambi zake – mauti.**

"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti" (Warumi 6:23).

**4. Mtu hawezi kujiokoa mwenyewe kwa sababu mwenye dhambi amekwisha kufa kifo cha kiroho. Tunasoma katika Biblia kwamba kabla mtu hajapata maisha mapya katika Yesu Kristo ni mfu katika makosa ya dhambi.**

"Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa ya dhambi zenu" (Waefeso 2:1).



Kama mtu ye yote aliyefariki kutokana na maradhi fulani hawezi kujifufua mwenyewe, vivyo hivyo, mtu aliyekufa kifo cha kiroho hawezi kujiokoa kutoka katika kifo hicho hicho cha kiroho.

## MUNGU AMEWEKA NJIA KWA AJILI YA WOKOVU WA MWANADAMU

**1. Njia hii ya wokovu ni Yesu Kristo.**

Watu wengi hutambua kwamba hawawezi kujiokoa wenyewe na ni lazima wasaidiwe. Walakini, wanakosea kwa kwenda kupata msaada kutoka pale usipoweza kupatikana. Wengine wanaamini katika ubatizo wao. Wengine wanategemea kuwa washiriki wa kanisa, na wengine wanaamini katika unabii wa uwongo. Tena kuna wengine wanaoamini katika uchawi na sanamu. Mungu ameweka tayari njia moja ya wokovu kwa watu wote ulimwenguni, njia hiyo imo katika Yesu Kristo. Ni Yesu pekee, ambaye anaweza kutuokoa kutoka dhambini na ghadhabu ya milele katika jehanam.

"Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima, mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi" (Yohana 14:6).

"Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo" (Matendo 4:12).

**2. Njia ya wokovu hupatikana katika kifo cha Yesu msalabani kwa ajili ya wenye dhambi wote.**

"Sisi sote kama kondoo tumepotea; Kila mmoja wetu amegeuka njia yake mwenyewe; Na Bwana ameweka juu yake Maovu yetu sisi sote" (Isaya 53:6).

"Kama vile Mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi" (Mathayo 20:28).

"Kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi" (Mathayo 26:28).

"Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye" (2 Wakorintho 5:21).